SUPA JACKPOT
TZS.1,042,026,796
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

## RC awataka DC na DED wajitafakari




UKURASA 13

Nipashe
Jumamosi Oktoba 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581106
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kikosi Kazi chaja na hoja nzito 18

**ZIMO** matokeo ya Uchaguzi Mkuu kuhojiwa mahakamani, kuondoa kinga ya Rais kushtakiwa. Samia anena...*Endelea uk. 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea ripoti ya kikosi kazi kuhusu uratibu maoni ya wadau wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa kutoka kwa Mwenyekiti wa Kikosi Kazi hicho, Prof. Rwekaza Mukandala, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mgongo wakwamisha kesi kina Mdee kortini

UKURASA 4

## Aua mke, ajinyonga kisa wivu

UKURASA 7

MICHEZO SIMBA YABADILI GIA, YANGA YAWASHTUKIA UK. 32
KATUNI UK. 6



Rais wa Zanzibar Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akisalimiana na Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Salmin Amour Juma (Komandoo), alipofika nyumbani kwake, Kijiji cha Kidombo, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana, baada ya kujumuika na viongozi na waumini wa Dini ya Kiislamu katika Hitma na Dua maalum ya kuwaombea Wazee. **PICHA: IKULU**

# Kikosi kazi chaja na hoja nzito 18

**Na Romana Mallya**

KIKOSI Kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi kimekabidhi ripoti yake kwa Rais Samia Suluhu Hassan kikiwa na mapendekezo 18 ikiwamo matokeo ya urais kuhojiwa mahakama ya juu.

Akiwasilisha maoni na mapendekezo hayo jana, Ikulu, jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kikosi Kazi hicho, Prof. Rwekaza Mukandala, alitaja pendekezo la kwanza kuwa ni kuruhusiwa kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa kama ilivyo kwa mujibu wa katiba na sheria.

Kikosi kazi hicho kimependekeza mikutano ya ndani ya vyama vya siasa iendelee kufanyika bila vikwazo vyovyote, yafanyike marekebisho ya sheria ili kuhakikisha mikutano ya hadhara inafanyika kwa ufanisi.

Pia alisema sheria ya vyama vya siasa ifanyiwe marekebisho ili kulipatia baraza la vyama vya siasa linaloundwa na vyama vyenyewe, mamlaka ya kushughulikia suala la uvunjifu wa maadili ya vyama kupitia kamati ya maadili. Sambamba na hilo, kikosi kimependekeza Msajili wa Vyama vya Siasa aandae mwongozo wa uchaguzi wa ndani wa vyama vya siasa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, pendekezo la tatu ni kuendelea na mfumo wa sasa wa kugawa ruzuku kwa vyama vya siasa, isipokuwa asilimia 10 ya fedha zinazotolewa ziwe kwa mgawanyo sawa kwa vyama vyenye usajili kamili.

Pendekezo la nne ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutolazimishwa kufuata amri au maagizo ya mtu, idara yoyote ya serikali, chama chochote cha siasa, taasisi au asasi yoyote na utendaji wake uruhusiwe kuhojiwa kwenye mahakama ya juu ili kuongeza uwajibikaji.

Mukandala alitaja la tano ni wajumbe wa tume ya taifa ya uchaguzi kuteuliwa na kamati inayoongozwa na Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji Mkuu wa Zanzibar, kamishna wa sekretarieti ya maadili ya viongozi wa umma Tanzania.

Wengine wenye jukumu hilo kwa mujibu wa mapendekezo hayo ni Mwenyekiti wa tume ya maadili ya viongozi wa umma ya Zanzibar, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na wajumbe wawili watakaoteuliwa na Jaji Mkuu wa Tanzania, baada ya kupendekezwa na vyama vya wanasheria Tanganyika na Zanzibar. Kikosi kazi hicho kimependekeza, angalau wajumbe wawili wa uteuzi wawe wanawake na sifa za kuwa mwenyekiti, makamu au mjumbe ziainishwe. Pia nafasi za ujumbe zitangazwe, watu wafanyiwe usaili na majina yapelekwe kwa Rais kwa uteuzi.

Jambo la sita, ni matokeo ya Rais yahojiwe Mahakama ya Juu huku pendekezo la saba likiwa wasimamizi wa uchaguzi wazingatie sheria, maadili, weledi, uwazi na ushirikishwaji wa wadau wakati wa kufanya kazi zao na watakaokiuka wawajibishwe kwa mujibu wa sheria.

Pendekezo la nane ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kupewa fedha kwa wakati ili kutelekeza majukumu yake ipasavyo.

Kikosi kazi hicho, katika pendekezo la tisa, kimetaka itungwe sheria ya kusimamia shughuli za tume ya uchaguzi na kuwe na sheria moja tu ya kusimamia uchaguzi badala ya mbili ilivyo sasa.

Pia imependekezwa maofisa wa uchaguzi watakaoengua wagombea bila kuzingatia sheria na weledi, wawajibishwe kwa mujibu wa sheria.

Jambo la 10 lililopendekezwa ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye uchaguzi yaboreshwe na kuongezwa huku pendekezo la 11 likiwa ni sharti la uwapo wa sera ya jinsia kwenye kila chama cha siasa na ujumuishi wa makundi maalumu. Kadhalika, utaratibu wa uwakilishi wa viti maalumu uendelee isipokuwa sheria ziboreshwe kuweka ukomo wa miaka 10.

Pendekezo la 12 ni kuhusu sheria zinazokwamisha ushiriki wa watu wenye ulemavu kwenye siasa ziangaliwe upya na pendekezo la 13 ni juhudi za ushirikishwaji wa vijana kwenye siasa ziongezwe.

Katika pendekezo la 14, serikali imeshauriwa kuongeza utoaji elimu ya uraia kwenye ngazi zote za elimu na mtaala uzingatie elimu ya uraia na mpigakura.

**RUSHWA KATIKA KATIBA**

Prof. Mukandala alitaja pendekezo la 15 ni rushwa kutamkwa katika katiba ya nchi ili wananchi watambue kuwa vitendo hivyo havitavumiliwa wala kuonewa muhali.

Pia Katiba ya chama cha siasa iwe na adhabu ya kumwondoa katika mchakato wa uchaguzi mgombea aliyedhaminiwa na chama iwapo atathibitika kujihusisha na rushwa.

Jambo la 16 lililopendekezwa ni kuanzishwe utaratibu wa mijadala kila mwaka itakayohusisha viongozi wakubwa wa kitaifa na kisiasa ili kudumisha mshikamano na mahakama iwe ni mamlaka ya mwisho ya kuamua pindi maridhiano yanapokwama.

Pendekezo la 17 ni wanahabari kuunda chombo cha kuwasimamia pamoja na vyombo vyao, vyombo vya umma vitoe muda sawa wa kutangaza habari za wagombea wa vyama vyote kwa usawa. Pia uwapo mchakato wa wazi wa kuwajibisha vyombo vya habari badala ya kufungiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO).

Aidha katika jambo hilo, imependekezwa kuwa sheria zinazoratibu uhuru wa vyombo vya habari ziboreshwe ili kukuza uhuru wa habari na demokrasia.

Jambo la 18 ni mchakato wa katiba mpya uendelee na mjadala wa kitaifa kuhusu suala hilo uanze kabla ya kuanza kwa mchakato wa kuandika katiba mpya ili kujadili masuala ya msingi kama Muungano, mamlaka ya Rais, madaraka ya serikali za mitaa, rushwa na mfumo wa uchaguzi.

Kadhalika, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya Kura ya Maoni zihuishwe pamoja na kuundwa kwa jopo la wataalamu ili kufanya mapitio ya katiba inayopendekezwa kwa kuzingatia hali ya sasa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kikosi kazi hicho ambacho kimefanya kazi kwa miezi 10 kiliundwa na Rais Samia baada ya mkutano wa siku tatu uliofanyika kuanzia Novemba 15, mwaka jana, uliohusisha wadau wa demokrasia na vyama vya siasa jijini Dodoma. Katika mkutano huo, maoni na mapendekezo 98 yalitolewa.

## ...msimamo wa Samia

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amepokea mapendekezo ya Kikosi Kazi cha Kuratibu Maoni ya Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi, akiahidi kuyafanyia kazi na kusisitiza yaliyopendekezwa sio amri kwa serikali.

Akipokea mapendekezo hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais alisema kikosi kimefanya kazi kubwa huku la katiba peke yake likiwa ni kazi nzito.

Alisema watapanga vikosi kadhaa vikihusisha wanasheria, wanasiasa na kushirikisha baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo ili kuyafanyia kazi yaliyowasilishwa.

Alisema yapo baadhi ni mepesi ambayo yanaweza kufanyiwa kazi haraka na mengine wanatakiwa wakae waangalie sheria zilizopo zina upungufu upi na wanazibadilishaje kutokana na yaliyopendekezwa.

"Sio jambo kwamba leo tumekabidhiwa, kesho tunaanza kutekeleza maoni ya Kikosi Kazi, hapana! Kikosi Kazi kimetupa mambo mazuri ya kuyazingatia na kuyafanyia kazi kwenye mambo yetu ya serikali.

"Tumepokea na tutayafanyia kazi, kama ingewezekana tungedurufu nakala nyingi katika dhana ileile ya uwazi na ukweli tukazitoa, marekebisho ya kikosi kazi, lakini wananchi wakaelewa kwamba maoni ya kikosi kazi si mwisho. Si amri kwa serikali, kwamba lazima mfanye hivi kikosi kazi kimesema.

"Tutaitana tena tuangalie hali halisi ndani ya serikali na hali halisi ya sheria zetu nyingine, ili tuzifanyie kazi vizuri. Mengi ni marekebisho ya sheria," alifafanua.

Pia alisema wamepokea marekebisho ya ndani ya vyama vya siasa na kueleza kuwa na wenyewe (vyama vya siasa) wasiwe hodari kuirekebisha serikali tu, wajitizame wanavyokwenda.

"Watizame mambo ya usawa wa kijinsia yapo? Mambo ya matumizi ya fedha yapo? Mambo ya utawala yapo? Maana mwingine akishapata chama cha siasa anasema ni chake na si cha wanachama," alisema.

Pia, alionyesha kufurahishwa na kikosi kazi hicho ambacho ndani yake kuna wanasiasa ambao nao wameona wachambue wanakwendaje.

Rais pia, alikubaliana na kamati hiyo kuhusu mambo ya jinsia ndani ya vyama vya siasa na kueleza kuwa chama chake kiko vizuri kuliko vyote na kutaka vingine viende katika misingi hiyo.

"Makundi maalum ninakubaliana nalo, yamependekezwa mambo mengi ambayo yanaleta athari ya gharama kwa serikali, tutakwenda kutekeleza yale ambayo ukiyatekeleza yanaleta matokeo makubwa kwa jamii.

"Haya mengine yanayohusu gharama yatategemea hali ya uchumi na hali ya mfuko wa serikali ilivyo mfano ruzuku kwa vyama vya siasa, itategemea hali ya mfuko ilivyo, tutatoa kulingana na mfuko, kama kugawana kwa misingi hii iliyoletwa na kikosi kazi, basi inabidi mfuko ule uguswe kwenye mpango mliosema.

"Hatuwezi kusema tutaingiza fedha zaidi, kwa sababu ni masuala ya bajeti, bajeti kwa mwaka huu ilishapita tunaangalia mwakani na pengine hata utekelezaji wake huenda ukaanza kwa bajeti za mwakani, ni wazo tumelipokea tutalifanyia kazi," aliahidi.

Kuhusu muungano wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Rais alisema watalikalia kitako na kusisitiza kuwa mambo yaliyopendekezwa na kikosi kazi ni mengi lakini hawawezi kuacha yote yanayotendeka serikalini na kujikita kutekeleza ripoti.

Kuhusu mapendekezo ya mijadala ya kisiasa kila mwaka, Rais Samia aliliomba Baraza la Kisiasa lifanye hivyo ili kujijadili na kuwataka wasijadili tu serikali na wao wenyewe.

Rais pia, alisema ripoti imegusia suala la rushwa ambalo aliliita kidonda ndugu na hakuna chama hata kimoja kilichonusurika katika hilo.

"Kuna chama kimoja ndugu yangu mmoja ananiambia 'walikuja wajumbe hali yangu ilikuwa mbaya, nikaenda kuwapokea mkutano upo Dar es Salaam' akaenda hadi Chalinze mabasi ya wajumbe yanakuja, kaingia kawapiga mshiko, kawapiga chakula, kawaambia haya nifuateni gari lake lipo mbele mabasi nyuma hadi hoteli kubwa akawalaza siku ya pili kura zimemiminika, rushwa pia hakuna chama ambacho hakifanyi, mfano niliotoa huu si chama changu ni kingine," alisema.

Alisema lazima walivalie njuga suala la rushwa kwa kuanza wao wenyewe wapiga kelele (vyama vya siasa), ili wajirekebishe kwa kuwa watu wanakosa maadili.

Kuhusu mikutano ya kisiasa, Rais alisema ni lazima wazitupie jicho sheria na kanuni za mwaka 2019 kwanza ndipo ruhusa itoke kwa kuwa hawataki kurudi walikotoka.

## Mtaka aonya wasichana kupata maradhi sababu vidonge kuzuia mimba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewaonya wanafunzi wa kike na wasichana wanaotumia vidonge vya kuzuia ujauzito kwamba wako katika hatari ya kupata maradhi mbalimbali yakiwamo kansa na ugumba.

Mtaka aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha utiaji saini mikataba ya lishe kilichofanyika mkoani hapa.

"Niliwahi kuonana na watu wa UNFPA (Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu) kwenye suala la uzazi wa mpango nikawaambia ninakubaliana kabisa na uzazi wa mpango lakini nikawaambia hebu tumsaidie mtoto wa kike atimize malengo yake kwenye elimu.

"Nilisema hivyo kwa sababu mtoto wa kike ambaye hakusoma kabisa, mtazamo wake wa kuzaa watoto ni tofauti na aliyesoma miaka saba. Mtoto wa kike aliyemaliza miaka 12 shuleni mtazamo wake wa kuzaa ni tofauti na mtoto wa darasa la saba. Ni nadra sana kumkuta aliyemaliza chuo akazaa watoto 12," alisema.

"Niliwaambia UNFPA najaribu kufikiri mtu ambaye anakunywa dawa za kuzuia mimba akiwa kwenye ujana darasa la sita, anywe hizi dawa miaka sita ya sekondari, miaka mitatu ya digrii. Kuna mtu hapa ana dozi tumboni ya miaka 10 anakunywa vidonge vya majira. Mimi si mwanasayansi, tunakuja kupata kansa na ugumba ambao hauna kichwa wala miguu huko tunakokwenda," aliongeza.

"Na kama hapa Njombe mlivyofanya hizi hosteli zitasaidia sana watoto. Hizi hosteli tulizonazo leo mtoto wa kike akifanikiwa kwenye malengo yake miaka 12 tu uzazi wa mapango unawezekana kwa sababu anakuja kwenye ndoa baada ya kidato cha nne, anafahamu watoto wangu wawili, watatu, wanne wanatosha."

Mtaka alisema suala la afya linalosimamiwa na Rais Samia Suluhu Hassan lizungumzwe kwenye ukweli kwa kuwa wanafunzi wanaohubiriwa jambo hilo bado wadogo.

"Binti anaambiwa P2 ni sawa au si sawa kwenye wakati upi, muongelee mtoto ambaye ni mdogo anaanza kutumia P2 mpaka kwenye umri wa kupata mtoto. Mwangalie kijana ambaye ni mdogo anaanza kujifunza kutumia vumbi la kongo toka anabalehe mpaka anapata ndoa kwa hiyo kuna changamoto kubwa kwenye kizazi hiki kubwa sana" alisema.

Anaongeza kuwa "Ndoa maana hapa nimewatania kwamba nini kinaleta udumavu,tumbo au mbegu zenye udumavu,mtindo wa maisha hawa mabinti ukiwa mjamzito unatengenezewa suruali hawataki kuachia mtindo.Ukipata ujauzito na jinzi ya ujauzito ipo ni mjamzito lakini anajinyima kula hataki anaogopa kula asije kunenepa anapojifungua pia anajinyima hataki kunenepa"alisema.

Alisema kwa upande wa watoto wa kiume pia kuna changamoto kwa sababu wanatumia dawa za kuongeza nguvu za kiume pindi wanapobalehe hadi 30.

"Kuna kijana wa kiume amebalehe anaanza kunywa viagra, vumbi la Kongo, supu ya pweza na alkasusu anakuwa amekwisha nguvu. Hebu angalia moyo huu umeusisimua kwa dawa za kuongeza nguvu za kiume toka unaanza ujana mpaka miaka 35 utapata shida ya figo, shida ya moyo," alisema Mtaka.

Naye Ofisa Lishe Mkoa wa Njombe, Bertha Nyigu, alisema kuna changamoto kubwa ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano.

# RC awataka DC, DED kujitafakari

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

Mkuu wa mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, amemtaka Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, Tano Mwera na Mkurugenzi Mtendaji wa Halimashauri ya wilaya hiyo, Shafii Mpenda, kujitafakari kutokana na kushindwa kukamilisha kwa wakati miradi ya afya inayotekelezwa wilayani hapa.

Sendiga, alitoa agizo hilo jana kwa nyakati tofauti alipofanya ziara ya kikazi kukagua miradi ya afya inayotekelezwa wilayani hapa pamoja na kuzungumza na wananchi ili kusikiliza na kutoa majibu kero zinazowakabili.

Alisema amekagua maendeleo ya ujenzi wa vituo vya afya vya Kanyezi kinachojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 400, Legeza Mwendo kinachojengwa kwa Sh .mlioni 700 lakini bado havijakamilika.

Mkuu wa mkoa alivitaja vituo vya afya vingine kuwa Mwazye kinachojengwa kwa Sh. milioni 500 pamoja na Hospitali ya Wilaya ya Kalambo inayojengwa kwa Sh. bilioni tatu ambavyo kwa pamoja vimeshatumia zaidi ya Sh. bilioni 4.6 lakini huduma bado hazijaanza kutolewa.

Alisema ujenzi wa vituo vya afya ulianza tangu mwaka 2018 na sasa ni miaka mitano haujakamilika na serikali imekuwa ikitoa fedha na kwamba amebaini kuwa tatizo ni viongozi na watendaji wa serikali ya wilaya kutosimamia vizuri.

"Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi lazima mkae chini na kujitafakari wilaya hii ina shida gani?, Kalambo kuna shida kubwa miradi haikamiliki kwa wakati. Siwezi kukubali kuona miradi inakwama wakati wananchi wanahitaji huduma," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alitoa siku 14 kwa viongozi wa wilaya hiyo wahakikishe huduma za afya zinaanza kutolewa kwenye vituo hivyo vya afya ili wajawazito na watoto wapate huduma karibu na maeneo wanayoishi. Kwa mujibu wa taarifa ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo iliyotiwa saini na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, Sunday Wambura vituo hivyo vilianza kujengwa mwaka 2018 na mpaka sasa ni miaka mitano lakini havijakamilika na huduma bado hazijaanza kutolewa.

Naye Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Legeza Mwendo, Emmanuel Matinda, alisema changamoto kwenye miradi hiyo ya afya ni upatikanaji wa fedha za ndani za halmashauri ili kukamilisha kazi ndogo kama mifumo ya maji taka, umeme na jengo la upasuaji ili huduma zianze kutolewa.




Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Juma Kipanga (katikati), akipokea zawadi kutoka kwa mnufaika wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF), Esther Shebe, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima nchini katika viwanja vya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TEA yatakiwa kuwafikishia mafunzo kuendeleza ujuzi Watanzania wengi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeitaka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kuhakikisha mafunzo ya kuendeleza ujuzi yanawafikia Watanzania wengi nchini na imepongeza namna wanufaika wa mafunzo hayo walivyofanikiwa kuanzisha biashara zao.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Juma Kipanga, wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima nchini yaliyofanyika kwenye viwanja vya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Dar es Salaam.

Mafunzo ya kuendeleza ujuzi yanafadhiliwa na Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) na kusimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na mpaka sasa jumla ya watu zaidi ya 36,000 wameshanufaika nayo.

Akiwa kwenye banda la TEA, Naibu Waziri Kipanga alizungumza na wanufaika wa mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi, Esther Shebe ambaye ni mkulima wa Uyoga jijini Dar es Salaam na Azalia Madege ambaye alipata mafunzo ya kuendesha na kutengeneza pikipiki za miguu miwili na mitatu na kwa sasa ameajiriwa katika kampuni ya kuagiza na kuuza pikipiki ya Fekon kama fundi.

Naibu Waziri alielezea kufurahishwa na namna mafunzo hayo yalivyowafikia wananchi wengi na kumudu kuondokana na umaskini kwa kuanzisha biashara zao na kuagiza mafunzo hayo yawafikie watanzania wengi kama sehemu ya kutatua changamoto ya ajira.

Kipanga alisema, serikali inafurahia mchango wa mfuko huo kwani vijana wengi watakaopata mafunzo kama hayo watajiajiri na kuajiri wenzao hali itakayosaidia kupunguza malalamiko ya ukosefu wa ajira nchini.

Mratibu wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF), Masozi Nyirenda, alisema SDF ni sehemu ya Programu ya Kuendeleza Elimu ya Ujuzi na Mafunzo ya Stadi za Kazi zenye kuleta tija katika Ajira (ESPJ) na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza na Kuendeleza ujuzi nchini (NSDS) ambayo inasimamiwa na (TEA) na inafadhiliwa na Serikali pamoja na Benki ya Dunia (WB).

Alisema, tangu kuanzishwa kwake, zaidi ya wananchi 36,870 wamenufaika na ruzuku ya Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi ili kuwawezesha kujiajiriwa au kujiajiri wenyewe.

Nyirenda alisema, awamu ya kwanza ya SDF ilianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo Taasisi 15 zilifadhiliwa kwa jumla ya Sh.Bilioni 3.1 wakati katika awamu ya pili Taasisi 81 zimenufaika kwa ufadhili wa kiasi cha Sh.Bilioni 9.7 zikitumika kuendesha programu za mafunzo ya ujuzi.

KESI KINA MDEE:

# Mgongo wamkwamisha mbunge kuhojiwa kortini

**Na Grace Gurisha**

MBUNGE wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Grace Tendega ameshindwa kuendelea kuhojiwa na mawakili wa chama hicho katika

Mahakama Kuu Masijala Kuu kwa madai anaumwa mgongo.

Tendega, alidai hayo jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama hiyo kupitia mawakili wake, Ipilinga Panya na Aliko Mwamanenge katika kesi kupinga kuvuliwa uanachama iliyofunguliwa na Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18.

Kutokana na taarifa hiyo, Hakimu Mkeha aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 3, 4, 8 na 9 mwaka 2022 kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa na kuhojiwa kwa Tendega kwa sababu Oktoba 13, 2022 hakumaliza kuhojiwa na mawakili wa CHADEMA,

Jaji Mkeha pia alipanga kusikilizwa kwa kesi hiyo tena Desemba 6 na 7 mwaka 2022 kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji kwa sababu wabunge wengine wanne hawajahojiwa kuhusiana na viapo vyao walivyoviwasilisha mahakamani huko.

Awali, Tendega alidai mahakamani kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika alikwenda katika kikao chake akiwa na majina 10 ya wabunge wa viti maalum huku akipendekeza kwamba katika majina ya wateule lazima awapo Nusrat Hanje.

Alidai kuwa Novemba 7, 2020 yeye kama kiongozi wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) alikuwa kwenye kikao ambapo siku hiyo kulikuwa na vikao vingi vya kuchagua wabunge wa viti maalum.

Tendega alidai wakati wanaendelea na kikao hicho, aliingia Mnyika akiwa na majina yake 10 ya wateule wa viti maalum huku akisisitiza katika wateule hao lazima awapo Nusrat Hanje kwa sababu yupo mahabusu, hivyo awapo ili aweze kutoka huko.

Hata hivyo, katika video ambayo imechezwa mahakamani huko, ilimwonesha Mnyika na Mwenyekiti wa Chama hicho, Freeman Mbowe wakidai kuwa Kamati Kuu haikuwahi kupitisha majina 19 ya wabunge hao.

Huku Mnyika akidai kuwa Novemba 23, 2020 Hanje alitolewa mahabusu ili watimize adhima yao ya kuapishwa kwa Mbunge huyo Novemba 24, 2020.

Mdee na wenzake 18 walifungua kesi hiyo Julai 21 mwaka huu mahakamani huko dhidi ya CHADEMA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wakipinga uamuzi wa Baraza Kuu la chama hicho kuwavua uanachama Mei 11, mwaka 2022.

Katika shauri hilo namba 36 la mwaka 2022, wabunge hao pamoja na mambo mengine, wanaiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi huo wa Chadema kuwafukuza, kisha itoe amri tatu.

Wabunge hao wanaomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na amri ya zuio dhidi ya Spika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutokuchukua hatua yoyote mpaka malalamiko yao yatakapo amuriwa.




Mkaguzi Mkuu wa Ndani Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (wa tatu kushoto), akikabidhi kiti kama ishara ya msaada wa viti 50 na meza 50 vyenye thamani ya Sh. Milioni 5 kwa Makamu Mkuu wa shule ya sekondari Mzumbe, Edwin Matenga (wapili kulia), wakati wa mahafali ya 62 ya shule hiyo, mkoani Morogoro juzi. Wengine ni Mkuu wa mkoa wa Tanga, Omari Mgumba (kushoto), Mwakilishi wa wazazi wa wahitimu na Meneja wa benki hiyo tawi la Wami, Harold Lambileki na (kulia) ni Diwani wa kata ya Mzumbe, Godfrey Lumungoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB kuendelea kuipiga jeki serikali sekta elimu

**Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

UONGOZI wa Benki ya NMB umesema umekuwa ukiwajibika kwa jamii kila mwaka ikiwa ni sehemu ya mikakati yake kusaidiana na serikali kuweka mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia kwa kutoa msaada wa vifaa vya elimu katika shule za msingi na sekondari nchini.

Akizungumza katika mahafali ya 62 ya Shule ya Sekondari ya Wanafunzi Wenye Vipaji Maalum Mzumbe mkoani hapa, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa alisema jana kuwa benki hiyo imekuwa ikitoa vifaa mbalimbali kusaidia sekta ya elimu kila mwaka ili kuiunga mkono serikali kuboresha sekta hiyo.

Baragomwa alisema, benki hiyo imekabidhi viti 50 na meza 50 vyenye thamani ya Sh. milioni tano shuleni Mzumbe katika mahafali hayo ili kukabiliana na shida upungufu wa meza na viti kwa wanafunzi darasani.

"NMB imekuwa ikishirikiana na serikali katika kuweka mazingira bora ya kusomea na kufundishia kwenye sekta ya elimu nchini na leo (jana) Mzumbe Sekondari tumekabidhi viti 50 na meza 50 ili kukabiliana na shida ya upungufu wa vifaa hivyo na tupo katika mipango ya kuleta kompyuta hapa," alisema Baragomwa.

Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mzumbe, Edwin Matenga alisema shule hiyo imekuwa ikishika nafasi tofauti tofauti katika shule 10 bora za sekondari katika matokeo ya kidato cha pili, nne na sita.

"Wanafunzi katika matokeo ya mitahani ya taifa kidato cha pili, nne na sita wamekuwa wakifanya vizuri kwa kuwa katika shule 10 bora na tunashukuru Benki ya NMB kutoa msaada ya viti 50 na meza 50 kwa kutufadhili na umesaidia kuondoa changamoto kubwa ya thamani hizi," alisifu.

Matenga alisema licha ya mafanikio ya kitaalumu, kumekuwa na shida ya miundombinu kukaa ikiwamo vyoo, uchakavu wa nyumba za watumishi na kipindi cha masika kuwa na wasiwasi.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba ambaye ni mmoja wa wazazi wa wanafunzi wanaotarajia kuhitimu elimu ya sekondari katika shule hiyo mwaka huu, alisema baada ya kumalizika kwa mahafali hiyo, wanafunzi wana wajibu sasa wa kufanya maandalizi kwa ajili ya mtihani wa taifa kidato cha nne.

"Nimekuja kwenye haya mahafali Mzumbe Sekondari kama mzazi na niwapongeze uongozi wa Benki ya NMB kutumia mahafali hayo kutoa msaada wa viti na meza na hii ni fahari kwa serikali tasisi hii inaposaidia kutoa vifaa vya elimu katika shule za sekondari na msingi hapa nchini," alipongeza Mgumba.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kwa Mwaka 2020/21, mbali na mambo mengine, imeangazia uhaba wa miundombinu, samani na watumishi katika shule za msingi na sekondari nchini.

# Watoto 11,500 wafanyiwa ukatili nchini mwaka 2021

**Na Sabato Kasika**

WATOTO 11,499 walifanyiwa ukatili wa jinsia mwaka jana huku 5,899 kati yao wakinajisiwa, hivyo jitihada zaidi zinahitajika ili kukomesha vitendo hivyo nchini.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima alibainisha hayo juzi alipozindua jengo la ofisi ya Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam.

Kituo hicho kinajishughulisha na vita dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii, sasa kimejenga ofisi yenye thamani ya Sh. milioni 11 iliyozinduliwa na waziri huyo.

"Takwimu za mwaka jana zinaonyesha kuwa jumla ya watoto 11,499 walifanyiwa ukatili, ambapo 5,899 walibakwa, lakini asilimia 60, yaani zaidi ya nusu walibakwa majumbani kwao na ndugu zao," alisema Dk. Gwajima.

Waziri huyo alifafanua kuwa watoto 1,114 walilatiwa huku asilimia 60 wakiwa wamelawitiwa majumbani mwao na asilimia 40 walilawitiwa njiani wakienda shuleni katika magari ya shule, shuleni au maeneo mengine."Hapa ukigawanya kwa mwezi sasa, wastani ni kwamba waliobakwa ni 491, waliolawitiwa ni 93, lakini unaambiwa kwamba hao wote wengi hawakutoa taarifa sehemu yoyote, bali ni asilimia 12 tu waliotoa taarifa," alisema.

Waziri huyo alisema zimetengenezwa kamati za ulinzi dhidi ya ukatili wa kijinsia ambazo ni kamati za jamii na ziko kwenye mpango wa serikali wa mwaka 2017 hadi 2022 ambao unaendelea kwa miaka mingine mitano.

"Miongoni mwa kamati hizo ni hii ya Kipunguni, nimekuja kuitembelea, mimi si waziri wa kusoma karatasi, ni waziri wa jamii, ninafuatilia maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii, niyashike, niyapapase na niyashuhudie," alisema.

Waziri huyo alisema hawezi kukaa ofisi wakati anasikia kuna taarifa za kushamiri kwa ukatili ikiwamo kuuawa kwa baadhi ya watu kwenye jamii, watoto, wanawake na wanaume wakifanyiwa ukatili wa kijinsia.

Aliongeza kuwa wizara hiyo imeundwa kutetea watoto na kuna mabaraza yao, madawati ya ulinzi wa watoto shuleni na nje ya shule, huku akiahidi kuzunguka maeneo mbalimbali kukagua kama yanafanya kazi.

"Tutafanya kazi hata katika majumba ya watu, tukikukuta unamkatili mtoto tunashughulika na wewe huko huko na kisha tunakufikisha kwenye vyombo vya sheria, ili kukomesha vitendo hivi katika jamii," alisema. Akizungumzia ujenzi wa ofisi ya Kituo cha Sauti ya Jamii, Diwani wa Kipunguni, Steven Mushi alisema walinunua kiwanja kwa Sh. milioni tano kisha ujenzi ukagharimu Sh. 6.9.

"Ununuzi wa kiwanja na ujenzi tumetumia Sh. milioni 11.9, tumezingatia ujenzi wa gharama na nafuu ambapo jengo lina chumba cha ofisi na cha kutolea mafunzo ya ufundi cherehani na mengine ya ujasiriamali," alisema Mushi.

HABARI KITAIFA

# DC atoa siku saba kampuni kutoa mbolea

**Na Martha Sambo,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, ametoa siku saba kwa kampuni za pembejeo za kilimo wilayani hapa kuwapa mawakala mbolea ya ruzuku ili wakulima wapate kwa wakati.

Mkuu huyo wa wilaya alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na wawakilishi wa kampuni hizo zilizopata kibali cha kusambaza mbolea kwa mfumo wa ruzuku.

Moyo alisema hadi Jumatano ijayo, kampuni hizo ziwe zimeanza kutoa mbolea hizo kwa mawakala.

"Mtuambie kampuni kama mmeshindwa kazi haraka na mimi nawapa leo (juzi) hadi Jumatano muwe mmeshapeleka mbolea kwa mawakala ili wazifikishe kwa wakulima maana lazima mtii makubaliano mliyoingia na serikali," alisema.

Moyo alifikia hatua hiyo baada ya mawakala wa mbolea za ruzuku kuzilalamikia kampuni zilizoingia mkataba na serikali kutoa mbolea za ruzuku kwa mawakala zinazotakiwa kuwafikia wakulima kwa bei ya ruzuku.

Wakizungumzia mfumo wa uuzaji wa mbolea kwa mfumo wa ruzuku, wawakilishi wa kampuni za mbolea zilizopewa kibali na serikali kuuza mbolea hizo walisema wana hofu kutolipwa pesa zao na serikali huku wakishauri serikali kuwaongezea fedha ndipo waagize mbolea hizo nje ya nchi.

Lwiza Mchilasi, mmoja wa wauzaji wa mbolea hizo alisema: "Kutokana na madeni ya nyuma serikali kushindwa kulipa, kampuni nyingi zinaogopa kutoa mbolea hizo. Tatizo ni mfumo yaani madeni ya nyuma, lakini wakala akija na ana vigezo tunamhudumia kama kawaida. Kuna haja ya serikali kulitazama hili kwa upya ili kampuni ziwe na imani nayo."



Barabara ya mchepuko inayopita juu ya daraja la magari eneo la Mbezi Mwisho Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, ikionekana kukamilika ambapo inatarajiwa kupunguza msongamano wa magari katika Barabara ya Morogoro. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Bunge lataka serikali kuiwezesha TIRDO

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), imetaka serikali kuliwezesha kibajeti Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), ili kutimiza majukumu yake kwa ufanisi na kuondokana na kutumia sehemu ya maabara yake kama ofisi.

Akizungumza jana baada ya kukutana na shirika hilo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa, alisema: "Ukienda TIRDO pale Msasani (dar es Salaam) hata ofisi hawana wanazotumia sasa zilipaswa kuwa maabara. Wamekuwa wakiomba fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi," alisema.

Silaa alisema mwaka huu wametengewa Sh. milioni 650 lakini ni muhimu serikali kuongeza nguvu kwenye shirika hilo.

Kadhalika, alisema serikali kama ina nia ya kusaidia ukuaji wa sekta zote kupitia viwanda ni muhimu kuliwezesha kibajeti shirika hilo.

"Unapozungumzia kilimo chochote nchi hii bado inauza mazao ghafi nje ya nchi kama pamba, korosho, bila kuwa na TIRDO unaondoa chachu ya uanzishaji viwanda nchini," alisema.

Pia, alisema kamati inaona TIRDO ni roho ya kujenga uchumi wa viwanda na kushauri serikali kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye shirika hilo.

Alisema shirika hilo lilisaidia ujenzi wa viwanda vya serikali ambapo majukumu yake makubwa ni kufanya utafiti wa teknolojia zinazotumika viwanda.

"Katika dhamira ya kuleta mapinduzi ya viwanda shirika lilifanya utafiti wa viwanda mbalimbali ikiwamo cha kiwanda cha ngozi Kilimanjaro, kiwanda cha mazao mchanganyiko,"alisema.


## TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LTD

TANESCO

**Tender No. PA/001/2022-2023/HQ/C/023**

**For**

**Provision of Consultancy Services to Conduct Feasibility Study, Environmental and Social Impact Assessment (ESIA), Conceptual Design and Tender Document Preparation for 400kV Transmission Line from Kisongo-Same-Segera with Associated Substations**

**and**

**Tender No. PA/001/2022-2023/HQ/C/024**

**For**

**Provision of Consultancy Services to Conduct Feasibility Study, Environmental and Social Impact Assessment (ESIA), Conceptual Design and Tender Document Preparation for 220kV Transmission Line and Submarine Cables from Tanzania Mainland to Zanzibar Island (Unguja and Pemba) and Mafia district located in Pwani Region with associated substations**

**Notice to the Public**

***Date: 22/10/2022***

TANESCO hereby informs the public that, the submission deadline for the Expression of Interest for the above mentioned tenders has been extended to 7th November, 2022 at 10:30 AM, East African time.

The Terms of References have been uploaded to TANESCO website (**www.tanesco.co.tz**). Further be informed that all clarifications will be uploaded to TANESCO website and applicants may submit their proposals physically to the address indicated in the Expression of Interest Documents (also available in above website) or electronically through E-mail: **Sec.TenderBoard@tanesco.co.tz**

Tender opening ceremony will be held at TANESCO Ubungo, Ground Floor, Room No. G06 immediate after the closing date and time mentioned above in presence of applicants or their representative who wish to attend the opening ceremony. Minutes of the opening will be shared to all Applicants.

**MANAGING DIRECTOR**
**TANESCO LIMITED**

2117108302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serengeti Girls wanahitaji heshima, zawadi maalum

**TIMU** ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 maarufu kwa jina la Serengeti Girls leo wanatarajia kushuka dimbani kuwakabili Colombia katika mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Dunia (U-17), ambayo mwaka huu inafanyika nchini India.

Serengeti Girls ilitinga hatua hiyo baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi D, ikiwa na pointi nne mkononi, nyuma ya vinara, Japan waliojikusanyia alama tisa.

Wawakilishi hao wa Tanzania na Afrika Mashariki na Kati, walianza michuano hiyo kwa kupokea kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa mabingwa watetezi wa mashindano hayo, Japan halafu ikapata ushindi wa magoli 2-1 dhidi ya Ufaransa na mchezo wake wa mwisho wa hatua ya makundi ililazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Canada.

Timu hiyo inayofundishwa na Kocha Mkuu, Bakari Shime, si tu imeweka historia ya kufuzu fainali hizo kwa mara ya kwanza, lakini imeendelea kufanya vyema kwa kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali kwa kuwaondoa vigogo, Ufaransa na Canada ambazo zimekuwa na uzoefu na kushiriki mashindano hayo mara kwa mara.

Kufanya vizuri kwa timu hiyo ni kielelezo cha maandalizi mazuri na ya muda mrefu ambayo wameyapata wachezaji wa kikosi hicho ambacho kilianza kampeni yake kwa kuwaondoa Eritrea, Burundi na baadaye Cameroon.

Wakati wanacheza mechi ya mwisho ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali hizo, Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, aliwataka wachezaji wa timu hiyo kwenda kupambana bila woga kwa sababu wanakutana na nyota wenzao chipukizi, na hawaendi kuvaana na Samuel Etoo na wengineo waliowahi kuibeba Cameroon kwenye michuano mbalimbali.

Kiongozi huyo aliwahamasisha wachezaji waende katika fainali hizo kama washindani na si wasindikizaji, akiamini maandalizi waliyofanya kwa muda mrefu yanaweza kuwapatia matunda mazuri, jambo ambalo limetimia kwa kiwango cha juu.

Mafanikio ya Serengeti Girls hayajatokana na maandalizi ya zimamoto, bali yametokana na nguvu kubwa iliyowekwa na serikali ambapo ilishiriki kikamilifu kuhakikisha wanaweka kambi kwenye hoteli nzuri hapa nchini, kuanzia Dar es Salaam, Zanzibar na Karatu, kwa nyakati tofauti. Lakini pia serikali ilihakikisha timu hiyo inakwenda Uingereza kuweka kambi maalumu na baadaye kuelekea India kwenye michuano hiyo huku wachezaji na benchi la ufundi wakiwa na vifaa vya mazoezi vyenye ubora. Ikiwa huko pia ilipata nafasi ya kucheza mechi mbalimbali za kirafiki.

Mabinti hao wamefanya kile ambacho taifa ilikitarajia na ilikuwa ni ndoto ya kuona siku moja Tanzania inapata heshima kupitia mchezo wa soka kama ilivyowahi kutamba kwenye riadha na ngumi.

Ili kuwahamasisha wachezaji wengine chipukizi, huu ni wakati wa serikali kuwapatia zawadi ambazo zitawasaidia sasa wakiwa bado wachezaji, lakini pia hata pale watakapomaliza kusakata kandanda.

Kama ambavyo umri wao unawatambulisha, huu ni wakati wa serikali na wadau kuhakikisha nyota hao wanapata nafasi ya kuendelezwa kielimu kwa wale wanaosoma shule za sekondari na ambao wamemaliza pia kugharamiwa kujiunga na elimu ya juu kwa faida ya hapo baadaye.

Ni ukweli kwamba historia iliyowekwa na Serengeti Boys haitafutika, licha ya nyota hao kupatikana katika mazingira magumu, wametoka katika ligi yenye changamoto ya kukosa udhamini mnono au kwenye mashindano ya shule ambayo yanafanyika katika mikoa mbalimbali.

Wakati umefika kwa taasisi na makampuni mbalimbali kuwekeza katika soka la wanawake kwa sababu matunda na mafanikio yake yameshaonekana, heshima na historia yao itaendelea kubakia kwenye kumbukumbu mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.

Kila la kheri Serengeti Girls katika mechi ya leo dhidi ya Colombia, kila la kheri Tanzania ya Rais, Samia Suluhu Hassan.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tunataka kandanda safi, uchezeshaji bora 'dabi'

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara nyingine tena, kesho mashabiki wa soka Tanzania na Afrika nzima, watashuhudia mechi ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hii mara nyingi huvuta hisia za mashabiki wengi ambapo kabla kunakuwa na shamrashamra na tambo za hapa na pale, ili mradi tu kusherehesha mechi hiyo.

Imekuwa ni utamaduni wa enzi na enzi kila timu hizo zinapokutana kunakuwa na mbwembwe nyingi, tambo, vituko vya kila aina kiasi kwamba hata wale ambao si mashabiki wa soka au wafuatiliaji, wanatambua kama kuna mechi hiyo.

Ingawa kwa miaka ya hivi karibuni 'dabi' hiyo imeonekana kama haina vishindo kama miaka ya 1970, 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa ni huwa ni moja kati ya mechi zinazovuta hisia na kufuatiliwa zaidi na mashabiki wengi Ukanda wa Afrika Mashariki.

Mazingira ya mechi ya kesho ni kwamba Yanga inaingia uwanjani ikiwa imetolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Simba ikiwa imetinga kwenye hatua hiyo.

Hii inawafanya baadhi ya wachambuzi wa soka kuona kama Yanga ni kama wataingia wamenyo'ong'onyea, huku wenzao wakiingia wakiwa na nguvu.

Kwa upande wa pili ni kwamba Yanga itaingia kwenye mechi hiyo ikiwa inajiamini kwani kwa misimu ya hivi karibuni imekuwa ikiifunga Simba hata kama ikiwa kwenye kiwango duni.

Mara nyingi Simba imekuwa ikitoa sare. Mara ya mwisho Simba kuifunga Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu ni Februari 16, 2019 bao 1-0 lililofungwa na Meddie Kagere.

Kwenye mechi za jumla, Simba mara ya mwisho kuifunga Yanga ilikuwa ni Julai 25, 2021, Kombe la FA, Uwanja wa Lake Tanganyika Kigoma, bao la Thadeo Lwanga.

Ramadhani Kayoko ametangazwa kuwa ndiye atakayesimama katikati kuamua mechi hiyo, huku mwamuzi msaidizi namba moja akiwa ni Mohamed Mkono na Janeth Balama atakuwa ni mwamuzi namba mbili.

Si mara ya kwanza kwa mwamuzi huyo kuchezesha mechi za 'dabi' na kwa kiasi kikubwa ndiye mwamuzi pekee ambaye ameonekana kuimudu kwa kiasi chake.

Hata hivyo haiondoi tahadhari au ushauri kwa Kayoko na wenzake wanaokwenda kuichezesha mechi hiyo.

Kwanza kabisa wanachotakiwa kufanya ni kuitawala mechi na wachezaji wenyewe na si kutawaliwa.

Kuna baadhi ya waamuzi hukubali hata kusukumwa na wachezaji, lakini cha ajabu wamekuwa hawaonyi wachezaji hata kwa kadi ya njano.

Tunaona kwa wenzetu nje ya nchi, mchezaji kumgusa hata mwamuzi ni kosa kubwa.

Kwenye mechi kama hii ya 'dabi' ambapo wakati mwigine wachezaji hupatwa na jazba, mwamuzi anatakiwa yeye mwenyewe kuwa na kazi ya kuwatuliza au kushusha presha za wachezaji, wacheze soka la ushindani, kuvutia na kufurahisha mashabiki na si kusukumana au kuchezeana rafu.

Mara nyingi baadhi ya wachezaji hupatwa na jazba au hasira kutokana na mwamuzi mwenyewe kuwa na presha zaidi kuliko hata wachezaji wenyewe kwenye pambano.

Kayoko hatakiwi kuachia rafu zisizo na msingi wowote kwa kuhofia kutoa kadi, kwani tumeona mara nyingi waamuzi wanaofanya hivyo mwingine akirudishia pia anashindwa kuchukua hatua kwa sababu ya kwanza aliachia. Hii ndiyo inakuwa imewaingia wachezaji kwenye kuchezeana ubabe na mwamuzi kushindwa kuchukua hatua. Jambo hili lilikemewa hata na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo hivi karibuni akiwashangaa waamuzi kutokuwa na ujasiri uwanjani.

Pia Kayoko anatakiwa aiache mechi yenyewe iamue mshindi na si kutaka uwiano sawa, timu kama haipo vizuri kwa siku hiyo ifungwe idadi yoyote ya mabao na si kuonekana kuibeba timu ambayo inayoonekana inazidiwa kwa kuhofu kulaumiwa na mashabiki wao. Kama waamuzi wanachezesha haki na kuna timu siku hiyo haiko vizuri, ifungwe kutokana na udhaifu wao ili itakaporejea mazoezini ijisahihishe na si kuamua kuilinda ili isifungwe mengi.

Tunataka mechi ikiisha mashabiki wauzungumzie mpira na wachezaji si mapungufu ya waamuzi.

Tukumbuke kuwa Ligi ya Tanzania kwa sasa inatazamwa sehemu mbalimbali nje ya nchi, kwa hiyo wanaotazama soka, huwa wanaangalia pia uchezeshaji wa waamuzi.

# Amuua mke wake kisha kujinyonga

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

GETRUDA Paul (34), mkazi wa Kitongoji cha Mwamala, Kijiji cha Igumangobo, Kata ya Idukilo, Tarafa ya Mondo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, ameuawa na mumewe George Mahona (38) kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili ikiwamo kifuani na shingoni, chanzo kikitajwa wivu wa mapenzi.

Mume huyo anadaiwa kutekeleza mauaji hayo Oktoba 19 mwaka huu majira ya saa moja asubuhi katika kijiji hicho akimtuhumu mke wake kuwa na uhusiano wa nje ya ndoa kisha naye kujinyonga kutumia chandarua.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kaimu kamanda wa Polisi Mkoa Shinyanga, Leornard Nyandahu alisema taarifa walizozipata ni kuwa wanandoa hao walikuwa na mgogoro ambao mwanaume alikuwa akimtuhumu mke wake kuchepuka na mwanaume mwingine ndipo akafikia uamuzi wa kumshambulia mpaka kumuua.

"Tulipata taarifa ya tukio la mauaji ya Getruda Paul, aliyeuawa na George Mahona, ambaye ni mumewe kwa kumtuhumu mkewe kuchepuka na mwanaume mwingine ambaye hajajulikana. Baada ya kufanya mauaji hayo, mtuhumiwa huyo alichukua uamuzi wa kujiua kwa kujinyonga na kamba ya chandarua," alisema Nyandahu.

Alibainisha kuwa miili yote ilifanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Serikali Wilayani Kishapu na imekabidhiwa kwa ndugu zao kwa ajili ya taratibu za mazishi.

Alitoa wito kwa wanandoa wanapokuwa na migogoro watafute sehemu ya ufumbuzi wa matatizo yao na siyo kukaa kimya na mwisho wa siku wanajichukulia sheria mkononi na kusababisha mauaji.

Vilevile, Nyandahu alitoa wito kwa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi huku akibainisha mpango mkakati wa Jeshi la Polisi kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayevunja sheria huku upelelezi wa tukio hilo ukiendelea ili kubaini undani wake.



Wachuuzi wa samaki wakisubiri wateja katika eneo la Ukonga Banana, jijini Dar es Salaam jana. Samaki mmoja anauzwa kwa bei ya 5,000/- hadi 30,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kasi ya ukuaji NMB yawakosha wateja, waongezeka kwa zaidi ya asilimia 500

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Benki ya NMB wamekiri kuvutiwa na mafanikio yake kiutendaji hasa kasi ya ukuaji wake ambayo wengi wamesema ni sababu ya wao kuendelea kuwa waaminifu kwa benki hiyo.

Kwa kuzingatia hilo, wateja hao wamesema msimu huu wanasherehekea Wiki ya Huduma kwa Wateja Duniani kwa kutambua pia mchango wa benki hiyo na huduma zake kwenye mafanikio yao na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye hafla ya maadhimisho hayo zilizoandaliwa na benki hiyo kote nchini, wameishukuru benki hiyo kwa huduma bora na bunifu za kisasa. Pia wameipongeza kwa uimara wake na kusema kuenziwa na NMB imekuwa ni sehemu ya maisha yao na benki hiyo.

"Kwetu hii sherehe pia ni kwa ajili ya kutambua mafanikio ya NMB, uwezo wake mkubwa kifedha na uimara ilionao kiutendaji na kiuendeshaji," mwakilishi wa wateja wa tawi la Mlimani City, Shillah Mbogo, alisema hivi karibuni wakati Kanda ya Dar es Salaam ya NMB ilipoherehekea huduma.

Huko Babati mkoani Manyara, wateja wa NMB walisema benki hiyo inafanikiwa pia kwa sababu ya kuaminiwa na watu wengi, kitu kinachoifanya kuongoza kwa idadi ya wateja ambapo sasa hivi ni zaidi ya wateja milioni nne.

Kwa mujibu wa Aika Lema, NMB inawavutia wengi kutokana na uwekezaji wake endelevu kwenye miradi ya kijamii na ufadhili wa shughuli za jumuiya mbalimbali kama ilivyofanya siku kanda ya kaskazini kuadhimisha huduma kwa wateja.

Kupitia Mkuu wa Huduma Shirikishi, Valence Mtongole, NMB ilimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 22.

Ofisa huyo alisema kwao Wiki ya Huduma kwa Wateja ni zaidi ya kuwaenzi watu wanaoifanya NMB kuwa benki kubwa kuliko zote nchini kwani pia ni nafasi ya kupata maoni kuhusu huduma zao na jinsi inavyoendeshwa.

"Mimi mrejesho wangu kwenu kama kiongozi na mteja ni kwamba NMB ni mdau mkubwa wa maendeleo wa mkoa wetu," Makongoro alisema baada ya kupokea mchango wa mabati 600.

Aika, ambaye ni mfanyakazi wa kampuni ya Mati Super Brands Ltd, alisema NMB ni benki pendwa inayoweka maslahi ya wateja mbele lakini pia inayofuatiliwa kwa karibu sana.

"Inapopata faida tunajua, mapato yake yanaeleweka na mali zake zote ziko wazi. Kiufupi, huwezi kukwama ukiwa mteja wa NMB, kwa hiyo kuwa na msingi mpana wa wateja kwake ni rahisi," alibainisha.

Takwimu rasmi zinaonyesha kuwa wateja zaidi ya milioni nne iliyonao NMB sasa hivi ni ongezeko la zaidi ya asilimia 566 ya idadi ya iliyoanza nao biashara. Pia inajivunia ukwasi wa zaidi ya Sh. trilioni nane ukiligansha na mizania yenye ukubwa wa Sh. bilioni kadhaa mwaka 1997 ilipoanzishwa.

Kuna wakati NMB ilikuwa na matawi 97 tu. Sasa hivi yamefikia 228 yakichochea kukua kwake na kujiimarisha sokoni ambako pia ina ATM zaidi ya 800 na mawakala takribani 15,000.

"Nimekuwa mteja wa NMB tangu mwaka 2012 na tumekua pamoja. Nilipoanza kukopa nilipata TZS milioni 10 lakini sasa hivi nina sifa ya kukopa hadi TZS milioni 150," alibainisha mteja mwingine wa NMB Babati, Lydia Yahani Kasaini, ambaye ni Mkurugenzi wa Lemmy Enterprises.

Mikopo jumla ya NMB ilifikia Sh. trilioni 4.8 mwaka jana hii ikiwa ni mara mbili zaidi ya ukopeshaji wa mwaka 2015. Aidha, NMB imekuwa inafanya vizuri kuhamasisha upatikanaji wa amana za wateja ambazo sasa hivi ni zaidi ya Sh. trilioni saba.

Mwenyekiti wa Wajasiriamali wa Manyara, Ali Said Msuya, alisema yeye ni miongoni mwa wateja wanaovutiwa na jinsi NMB inavyotengeneza faida kubwa na kurudisha sehemu yake kwa jamii.

Kati ya mwaka 2015 na 2021, faida iliyopata NMB baada ya kodi ilipaa kwa zaidi ya asilimia 93 kutoka Sh. bilioni 150 hadi Sh. bilioni 290.

## KABWELA



# Puma Energy yazindua toleo la gesi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Puma Energy Tanzania Limited inayotoa huduma ya nishati nchini imezindua toleo lake la gesi ya 'Liquefied Petroleum' (LPG) jijini Dar es Salaam.

Pia imezindua ubunifu wake wa "PumaGas App" katika warsha na mafunzo kwa wafanyabiashara wake wa jiji hilo, ili kuonyesha jinsi inavyotoa urahisi kwa watumiaji na wasambazaji, huku ikiwahudumia watumiaji wengi zaidi kwa kutoa upatikanaji wa nishati ya gesi.

Katika mafunzo hayo, wafanyabiashara wengi walieleza kuwa ni jambo la kutia moyo kuona juhudi za Puma Energy za kuunga mkono lengo la kutoa huduma ya nishati ya gesi nchini Tanzania kwa kuanzia na Dar es Salaam, na baadaye kuenea katika mikoa mingi zaidi nchini.

Akizungumza katika warsha hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, Lameck Hiliyai, alisema Tanzania ni sehemu ya soko muhimu la kampuni hiyo na imejitolea kuchangia matarajio ya ukuaji wa nchi. "Serikali imeona ongezeko kubwa la matumizi ya LPG katika miaka kumi iliyopita, sekta hiyo imeshuhudia ukuaji wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kwa wastani wa zaidi ya asilimia 20 mwaka hadi mwaka kuanzia 2017 hadi 2021.

"Ni dhahiri matumizi ya LPG nchini Tanzania pia yameongezeka na kukua kwa kasi kwa miaka. Zaidi ya hayo, kutokana na kuendelea kwa maendeleo ya kiuchumi nchini Tanzania na kuongezeka kwa mwamko wa LPG kama njia bora zaidi ya kuni na mkaa, inatarajiwa kuendelea kukua hadi viwango vya juu zaidi mijini na vijijini. Kwa kuwa PumaGas sasa iko sokoni, itaunga mkono azma ya serikali ya Tanzania ya kuongeza matumizi ya LPG kote nchini," alisema.

Aidha alisema kuwa kampuni hiyo, imepanga kuendelea kuwekeza katika mtandao wake wa vituo vya rejareja na kupanua huduma zake kwa wateja na mafunzo hayo yanaakisi dhamira ya kuboresha ufikiaji wa suluhu za kutoa huduma ya gesi safi kote nchini.

"Pumagas App ni huduma bora kabisa ambayo itarahisisha huduma kwa watumiaji wengi na itarahisisha maisha ya kila mtu kwani imeundwa ili kuwarahisishia watumiaji wa gesi ya kupikia ambapo wateja wetu wanaweza kuagiza gesi moja kwa moja kwa simu zao kupitia msimbo wa USSD au kwa kupakua programu ya PumaGas ili kurahisisha upatikanaji wa gesi ya kupikia kuliko hapo awali," Alisema.

Alifafanua kuwa wazo hili bunifu lilitokana na azma yao ya kuunda suluhisho ambalo litawawezesha watumiaji wa LPG kupata gesi yao ya kupikia kwa urahisi wao, kwa wakati na vile vile kuwafikia nyumbani bila malipo.

"Tumehakikisha tunakuwa na wafanyabiashara wakubwa katika mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kuhudumia nyumba mbalimbali katika maeneo mbalimbali na baadae mwaka huu mtandao wetu utakua mikoa mingi zaidi ili kuhudumia kote nchini," alifafanua.



Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde (katikati), akifurahia jambo na Mkurugenzi wa JJAD Kagera Farmers Ltd, Dk. Albert Katagira (kulia), wakati wa uzinduzi wa ugawaji bure miche 3,000,000 ya kahawa aina ya Robusta kwa wakulima wa mkoa wa Kagera, katika kijiji cha Karenge, tarafa ya Kaisho, wilayani Kyerwa juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBAA yataja sababu wahasibu wengi kufeli

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), imetaja mambo yanayosababisha watahiniwa wengi kufeli mitihani ya bodi hiyo ikiwamo kukosa maandalizi ya kutosha kwenye vyuo wanavyosomea.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, Pius Maneno, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa bodi hiyo mwaka 1972.

Alisema NBAA haifundishi wahasibu na wakaguzi bali inafanya kazi ya kutunga na kusimamia mitihani kutokana na mitaala iliyopo, hivyo wanafunzi wasipoandaliwa vyema kwenye vyuo vyao wanaanguka kwenye mitihani.

"Watu wanalalamika kwamba mitihani yetu ni migumu. Ni kweli ni migumu lakini si kwa kiwango hicho kwa sababu wako wengi wanaofaulu. Mitihani inaonekana kuwa migumu kwa sababu anayefundisha siye anayetunga na anayetunga mtihani anaangalia mtaala, sasa kama hukuumaliza yeye hajui," alisema Maneno ambaye ni mhitimu ngazi ya CPA.

Alisema miaka ya nyuma NBAA ilikuwa inafundisha na kutunga mitihani lakini ilipofika mwaka 1991 iliamua kuachana na ufundishaji na kuachia sekta binafsi na yenyewe kubaki na jukumu moja la kutunga mitihani.

Maneno alisema hata Taasisi ya Uhasibu Arusha (AIA), ilikuwa chini ya usimamizi wa NBAA ambapo wanafunzi wanaosoma kwenye chuo hicho walikuwa wakimaliza na kwenda kufanya mitihani ya bodi hiyo wakati huo.

Maneno alisema baadaye NBAA iliamua kuirejesha serikalini taasisi hiyo ili ijiendeshe yenyewe kwani kuendelea kuwa chini ya bodi hiyo na kufanya mitihani inayotungwa na bodi haukuwa utaratibu mzuri.

"Tuliona kuna mgongano wa maslahi yaani ufundishe wewe na utunge mitihani wewe tukaachana na utaratibu huo ili watu wengine wawafundishe wahasibu sisi tutunge na kusimamia mitihani pekee, na kwenye kutunga tunaangalia kama mtahiniwa amesoma mtaala kwa asilimia 85" alisema na kuongeza

"Tatizo wakati mwingine unakuta mtahiniwa hajajiandaa vya kutosha na hajamaliza mtaala wote anakuja kwenye mitihani, sasa kama hajamaliza mtaala sisi hatujui kwa sababu kazi yetu ni kutunga mitihani na tunachotaka ni kupata wahasibu wa kiwango kile kile kwa wahasibu wa leo na wa zamani," alisema.

Alisema baadhi ya watu wanafanya mitihani ya bodi kutokana na shinikizo sehemu zao za kazi wakitaka kupandishwa vyeo lakini wanakosa maandalizi yanayotakiwa kwa ajili ya kufaulu mitihani hiyo.

"Mfano mtu kazini kwake kaambiwa bila kuwa na CPA huwezi kupanda cheo kwa hiyo anakurupuka kuja kufanya mitihani ya bodi ili apate CPA apande cheo sasa mitihani hii huwezi kufanya bila maandalizi ukafaulu kwa sababu unahitaji muda wa maandalizi," alisema.

Pia alisema wanafunzi wanapomaliza kusomea masuala ya uhasibu wanakwenda kupata mafunzo ya ziada ya kitaalamu kutoka kwa taasisi mbalimbali ambako wananolewa kabla ya kwenda kufanya mitihani inayosimamiwa na kutungwa na NBAA.

Alisema zamani fani hiyo ilipendelewa zaidi na wanaume lakini kadri miaka ilivyozidi kwenda idadi ya wanawake wanaosomea fani hiyo imekuwa ikiongezeka na kwa sasa kuna uwiano wa nusu kwa nusu kwa wasomi wa fani hiyo.

Alisema kwenye mahafali ya 44 yaliyofanyika hivi karibuni ambapo kulikuwa na wahitimu 1,115, idadi ya wahitimu wanawake ilikuwa sawa na ile ya wahitimu wa kiume hali ambayo alisema ni moja ya mafanikio ya bodi.

## Benki yakabidhi msaada madawati 100

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

KAMPENI ya ugawaji wa madawati 1,000 inayoendeshwa na benki ya Exim Tanzania katika mikoa mbalimbali nchini, imeonyesha mafanikio makubwa huku ubora wa madawati hayo ukiwavutia wakuu wa mikoa waliopokea, akiwamo wa Tanga, Omary Mgumba.

Akizungumza baada ya kupokea madawati 100 yaliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya mkoa huo juzi, Mgumba pamoja na kuonyesha kuvutiwa zaidi na ubora huo, alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka kwa kuwa mkoa kwa sasa uko kwenye mpango mahusus wa kukabiliana na uhaba wa madawati.

"Changamoto ya madawati katika mkoa wa Tanga ni kubwa licha ya jitihada tunazoendelea kuzifanya. Wilaya pekee yenye ahueni ni Pangani yenye uhaba wa madawati 400 huku wilaya ambayo inaongoza kwa uhaba ni Lushoto ikiwa na uhaba wa madawati 1,500 na hiyo ni kwa shule za msingi pekee, tunawashukuru sana Exim kwa msaada huu wa madawati ambayo ni bora zaidi," alisema Mgumba.


Mgumba pia alitoa wito kwa wadau mbalimbali mkoani hapa kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu katika kuleta maendeleo katika nyanja mbalimbali zikiwamo elimu na afya kupitia mipango ya uwajibikaji kwa jamii. "Tukimsaidia vyema Rais kupitia jitihada kama hizi zilizofanywa na benki ya Exim, tafsiri yake pia hata kasi ya maendeleo inaongezaka kwa sababu nguvu ambazo zingetumiwa na Rais na serikali katika ununuzi wa madawati, zinaelekezwa kwenye mipango mingine ya kimaendeleo," alisema Mgumba.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi madawati hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Exim, Jaffari Matundu, alisema msaada huo ni sehemu ya hitimisho la kampeni yao ya ugawaji wa madawati 1,000 iliyozinduliwa mwishoni mwa mwaka jana na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha miaka 25 tangu kuanzishwa kwa benki hiyo.

"Msaada huu wa madawati 100 hapa mkoani Tanga unaashiria mwanzo wa hitimisho la kampeni yetu ya ugawaji wa madawati 1,000 iliyofanyika kwa mafanikio makubwa. Mikoa yote ambayo tumekabidhi msaada huu ilionyesha kuvutiwa na ubora wa madawati haya yaliyotengenezwa kwa ubora wa hali ya juu ili kutumika kwa muda mrefu," alisema.

Aliitaja baadhi ya mikoa ambayo tayari imenufaika na msaada huo kuwa ni Dodoma, Mwanza, Lindi, Mbeya, Mtwara, Tabora, Shinyanga na Tanga.

Ofisa Elimu Mkoa wa Tanga, Newaho Mkisi, pamoja na kuishukuru Exim kwa msaada huo, alisema utasaidia kupunguza uhaba wa madawati katika baadhi ya shule zilizoko mkoani hapa ambazo kwa sasa zinakabiliwa na uhaba mkubwa kutokana na ongezeko la vyumba vya madarasa.



## SBL yatangaza neema kwa wakulima nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imetangaza neema kwa wakulima wa mahindi, shayiri na mtama nchini baada ya kuahidi soko la uhakika la mazao hayo.

Kwa sasa kampuni hiyo imesema imepanga kuanza kutekeleza mpango wake mahususi wa kununua takribani tani 20,000 za mazao hayo ya nafaka kwa mwaka kutoka kwa wakulima wa ndani.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Umma wa SBL, John Wanyancha, akizungumza jana katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, alisema kampuni hiyo inadhamiria kupanua uwanja wake wa ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima nchini, hasa katika mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Shinyanga, Mara na Mwanza ambako SBL imekuwa ikinunua mazao tangu mwaka 2013.

"Ni mpango mahususi wa kuwainua kiuchumi wakulima wa Tanzania. Tunaamini watapata faida na kubadilisha maisha yao kwa sababu tunakuja na mpango mahususi wa kununua malighafi ya mazao toka kwa wakulima wa ndani kwa ajili ya uzalishaji wa bia.

"Ongezeko la mahitaji yetu ya mazao kutoka kwa wakulima wa ndani ni dhumuni la makusudi la kupanua uwezo wa uzalishaji wa viwanda vyetu vilivyopo Moshi, Mwanza na Dar es Salaam. SBL imetumia takribani Sh. billioni 165 kwa miaka mitatu iliyopita kupanua uzalishaji viwanda vyake nchini," alisema.

Wanyancha alisema, wakulima wategemee kupatiwa mikataba mizuri, mbegu bure, mafunzo ya misingi ya fedha na mbinu za kisasa za kilimo kama faida mojawapo ya kufanya kazi na SBL.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu aliyepongeza juhudi za SBL kama mdau wa maendeleo nchini kupitia utoaji ajira kwa Watanzania, upanuzi wa nyenzo za maendeleo ya jamii kupitia programu zake na kuongeza mapato kwa serikali.

SBL ina takribani wafanyakazi 800 wenye ajira ya moja kwa moja na maelefu waliopo katika mnyonyoro wa thamani wakiwamo wakulima, wamiliki wa baa, kumbi za starehe na wasambazaji.

"SBL inasimama kidete kama mmoja wa wawekezaji makini katika uchumi na mkoa wetu (Kilimanjaro). Serikali iko makini na inaendelea kutoa ushirikiano katika kutengeneza mazingira mazuri ya kibiashara, ili kukuza uwekezaji na kuvutia wawekezaji zaidi kuja nchini Tanzania" alisema Babu.

# Fundi makenika jela maisha kwa kunajisi

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

FUNDI makenika, Leonce George (35) maarufu 'Simbaa', mkazi wa Kijiji cha Orngadida, Wilaya ya Babati mkoani Manyara amehukumiwa kutumikia kifungo cha maisha gerezani baada ya kutiwa hatiani na Mahakama ya Wilaya hiyo kwa kosa la kumnajisi mtoto mwenye umri wa miaka minane.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Victor Kimario alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo baada ya mtoto huyo (jina limehifadhiwa) kuitwa na mshtakiwa karibu na karakana iliyoko Babati na kisha kumnajisi, huku akijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

"Baada ya kupitia mwenendo wa shauri hili na kusikiliza ushahidi wa mashihidi wa upande wa mashtaka na upande wa utetezi, nimejiridhisha pasina shaka kwamba mshitakiwa alitenda kosa linalomkabili.

"Hivyo, mahakama hii inamhukumu kutumikia adhabu ya kifungo cha maisha jela kutokana na uzito wa kosa aliloshtakiwa nalo," alisema Hakimu Kimario. Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, Simbaa alidaiwa kutenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 130 (1) (2) (e) na 131 (3) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2019.

Mshtakiwa huyo anadaiwa kutenda kosa hilo Machi 14 mwaka huu kwa kumnajisi mtoto huyo aliyekuwa njiani, akitokea shuleni majira ya mchana.

Katika maelezo ya kosa, mshtakiwa anadaiwa kumwita mtoto huyo aliyekuwa akipita karibu na karakana na kumnajisi.

Anadaiwa kuwa mtoto huyo alipotii wito wa kuitwa na Simbaa, mshtakiwa alitumia upenyo huo kumpeleka mtoto pembeni mwa karakana na kumvua nguo na kisha kuanza kujinuisha kingono licha ya mtoto kulia kutokana na maumivu makali.

Baada ya mtoto huyo kufika nyumbani, alimweleza mama yake kilichotokea, ndipo mzazi huyo aliporipoti tukio hilo shuleni kwa walimu wake na kisha Kituo cha Polisi ambako mtoto alimtaja Simbaa kufanyia kitendo hicho.

Katika shauri hilo namba 54 la mwaka huu, upande wa mashtaka,ulikuwa na mashahidi wanne na upande wa utetezi ulikuwa na mashahidi wanne ambao katika ushahidi wao kwa namna tofauti walithibitisha kosa aliloshtakiwa nalo Simbaa.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Grace Mgaya aliiomba mahakama kumpa adhabu kali mshtakiwa ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Patrobas Katambi (kulia), akimpa mkono wa pongezi Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha Malt Super Brands Ltd, David Mulokozi kwa kutoa fimbo nyeupe 500 kwa watu wasioona, katika maadhimisho ya fimbo nyeupe Duniani kwenye Uwanja wa Kwaraa, Mjini Babati jana. Wa (pili kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Makongoro aiita TMDA kuzuia dawa feki mitaani

**Na Cynthia Mwilolezi,**
BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, ameiita Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) mkoani humo kuungana na maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama kupambana na wafanyabiashara anaowaita wakorofi wanaoingiza na kusambaza dawa feki za binadamu mitaani.

Kiongozi huyo alifikia uamuzi huo jana akiwa Wilaya ya Babati alipokutana na wataalamu wa afya na mifugo katika kikao kazi cha kujadili tatizo hilo linalohusu zaidi usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

"Nimewaita hapa ninyi wataalamu wa afya na mifugo kutoka Halmashauri zetu saba, mbele ya Kamati yangu ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Manyara ili tujadili jambo hili linaloendelea ambalo ni hatari kwa afya na ustawi wa wananchi wetu.

"Jukumu linalokuja mbele yenu kwa sasa ni pamoja na kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu watu wanaoingiza na kusambaza dawa bila ya kufuata Sheria ya Dawa na Tiba, Sura ya 219 ya Sheria ya Mwaka 2003. Nimekuwa nikipata taarifa juu ya TMDA kupitia vyombo vya habari jinsi inavyolinda afya ya jamii.

"Lakini pamoja na kukupongezeni, ninaagiza muendelee kufanya hivyo, huku mkiwawachukulia hatua za kisheria wale wote wanaokiuka sheria na kuhatarisha afya za wananchi kwa kukiuka sheria ya dawa na vifaa tiba," alisema.


Makongoro, akizungumzia suala la usalama na ubora wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, alitoa onyo kwa wanaokiuka masharti hayo hususani wanaouza bidhaa za dawa kwenye vyombo vya usafiri.

"Ninahimiza TMDA kuendelea kuwapa elimu na kuwachukulia hatua wakaidi, lakini nendeni nao taratibu kwa kuwapa elimu kisha hatua ifuate baadaye kwa wakaidi," aliagiza.

Akizungumza kuhusu taarifa hiyo, Kaimu Meneja wa TMDA Kanda ya Kaskazini, Dk. Furaha Nyunza alisema lengo la mamlaka hiyo ni kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa dawa na vifaa tiba vyenye ubora unaozingatia sheria.

"Mamlaka inahitaji utoaji na usambazaji wenye ubora unaozingatia misingi ya kisheria na sisi kama wasimamizi tutahakikisha malengo ya utoaji wa huduma yanazingatiwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

Hata hivyo, baadhi ya maofisa ugani idara ya mifugo wa Halmashauri za Simanjiro na Hanang wanasema kumekuwapo na shida hususani kwenye dawa za minyoo zinazosambazwa kutoka nchi jirani ya Kenya.



# RC ashtuka viongozi kutafuna fedha za lishe

Na Mary Mosha, MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu amesema analiona 'ombwe' la viongozi wenzake kujitwalia madaraka yasiyo ya kawaida ya kuchepusha fedha zinazotengwa kwa ajili ya masuala ya lishe, huku wakijua kufanya hivyo ni kukiuka maelekezo ya serikali.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza Halmashauri sita za mkoa huo ambazo ni Manispaa ya Moshi, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Hai, Siha, Rombo, Mwanga, Same, kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa mwaka huu zinatumika kama zilivyokusudiwa na si vinginevyo.

Babu alionyesha jana kukerwa na uchepushaji wa fedha za lishe na mafungu yake kuelekezwa katika matumizi mengineyo wakati hafla ya utiaji sahihi mkataba wa usimamizi wa shughuli za lishe.

"Leo (jana) ofisi yangu na wakuu wote wa wilaya tunatia sahihi mikataba ya lishe. Sitaki kusikia tena kuna wilaya imechepusha fedha kwenda kwenye miradi mingine badala ya lishe. Ninyi ni mashahidi kwamba Mkoa wa Kilimanjaro hivi sasa unashika nafasi ya 21 kati ya mikoa 26 katika suala la lishe.

"Tumeshuhudia katika mwaka wa fedha 2021/22, zipo baadhi ya halmashauri zimekuwa zikitumia fedha za lishe kwenye mambo mengine ambayo hayana uhusiano na masuala ya lishe. Sasa kwa mwaka wa fedha 2022/23 sitakubali kuliona hili tena," alionya.

Kwa mujibu wa Babu, kwa sasa mkoa umekuja na mkakati wa kuhakikisha unaondoka kwenye nafasi hiyo na kuingia katika 10 bora. Alitaja mmoja ya mkakati ni kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya lishe, zinatumika kama zilivyokusudiwa.

Mkuuwa Mkoa pia aliagiza halmashauri hizo kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za lishe, zinatolewa na kutumika kwa wakati.

Alisisitiza matumizi ya fedha za lishe yanapaswa kuzingatia bajeti na mpango wa matumizi, huku akiagiza Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za Serikali mkoani humo kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za lishe kila baada ya robo mwaka na taarifa hiyo ifikishwe kwa Katibu Tawala Mkoa huo.

Katibu Tawala Mkoa huo, Willy Machumu, akizungumza baada ya utiaji saini mikataba hiyo, alisema ili kujenga taifa lenye maendeleo, suala la lishe ni jambo la msingi katika jamii.

"Lishe si suala la kuchukulia la kupita njia, bali ni suala muhimu katika katika maendeleo ya taifa. Niwasihi sana waheshimiwa wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wakurugenzi wa halmashauri, mtekeleze makubaliano yaliyopo katika mikataba na msimamie utengaji wa fedha za lishe kulingana na idadi ya watoto," aliagiza.



Ofisa Forodha wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusta Kaunda (kulia), akitoa elimu ya kodi kwa mfanyabiashara wa wilayani Mafia, mkoani Pwani jana, katika kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango inayoendelea wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Jela miaka 30 kwa kumnajisi mwanawe

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

ELIHURUMA Mwandri (46), Mkazi wa Kijiji cha Lomakaa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, amehukumiwa kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela baada ya kutiwa hatiani na Mahakama ya Wilaya hiyo kwa kosa la kumnajisi mtoto wake wa kumzaa mwenye umri wa miaka saba.

Jana wakati Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Elibahati Petro, akisoma hukumu hiyo, alisema amelazimika kumpa adhabu hiyo mshtakiwa Elihuruma baada ya kuridhika na namna upande wa mashtaka ulivyofanikiwa kuijenga kesi hiyo ambayo ushahidi wake hauachi shaka yoyote.

"Nimepitia mwenendo mzima wa kesi hii na ushahidi uliotolewa na pande zote mbili, yaani upande wa mashtaka na upande wa utetezi nimejiridhisha pasipo shaka kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo, hivyo kwa mujibu wa sheria anahukumiwa adhabu ya kifungo cha miaka 30 gerezani," alisema.

Wakati anasoma hukumu hiyo, Hakimu Elibahati alisema upande wa mashtaka katika kesi hiyo ulikuwa na mashahidi watano, akiwamo daktari aliyefanya uchunguzi wa kitabibu, mwanaharakati, mama mzazi na mwathirika mwenyewe.

Kwa mujibu wa Hakimu huyo, mshtakiwa alikuwa akiishi na mwanaye huyo (jina limehifadhiwa) huku akiwa ametengana na mzazi mwenzake.

Alisema, malezi hayo ya upande mmoja yalimrahisishia mshtakiwa kufanya ukatili huo ambao ni kinyume cha Kifungu cha 130 (1) (2) (e) na kifungu 131 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2019.

Baada ya mshtakiwa kutiwa hatiani, mahakama hiyo ilimpa nafasi ya kujitetea ambapo mshtakiwa aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa sababu anaishi na mama yake mzazi ambaye ni kikongwe anayemtegemea kumtafutia chakula, vilevile yeye mwenyewe ni mgonjwa.

Katika maelezo ya kosa, ilidaiwa mahakamani huko kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Mei 16 mwaka huu katika Kijiji cha Lomakaa, Kata ya Kirua kwa kumnajisi mtoto huyo, huku akitambua kwamba kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo, Mwendesha mashitaka wa Serikali, David Chishimba, alidai mahakamani huko kwamba mtoto huyo akiwa Shule ya Msingi Lomakaa, alifichua ukatili huo wakati mwalimu wake akiwafundisha kuhusu madhara ya ukatili kwa watoto na namna ya kujikinga,

Mtoto huyo alimfuata mwalimu wake (jina limehifadhiwa) na kumweleza kuwa baba yake amekuwa akimfanyia ukatili kwa kumnajisi.

Kutokana na maelezo ya mtoto huyo, mwalimu wake alichukua jukumu la kutoa taarifa kwa mmoja wa wanaharakati na kisha mwanaharakati huyo kutoa taarifa Kituo Kikuu cha Polisi Sanya Juu ambako polisi walimsaka na kufanikiwa kumkamata mshtakiwa.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka huyo alisema, kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo katika jamii chisimba aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya mshitakiwa.

## Mtoto adaiwa kunajisiwa na rafiki wa baba yake

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

VISA vya ukatili wa kijinsia vinazidi kushika kasi katika Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, safari hii mwanafunzi wa kidato cha pili mwenye umri wa miaka 15 anadaiwa kunajisiwa kwa ahadi ya kupewa Sh. 2,000, kununuliwa simu janja na begi la shule.

Inadaiwa kuwa mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) kwa sasa amekatisha masomo yake baada ya kupata ugonjwa wa zinaa uliotokana na kufanyiwa ukatili huo na mtu anayedaiwa kuwa rafiki mkubwa wa baba yake mzazi.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Yahaya Mdogo, mtuhumiwa anayetajwa kufanya tukio hilo, Alfred Njau (38) alikamatwa Oktoba 8 mwaka huu na baadaye aliachiwa kwa dhamana. "Ni kweli tulimkamata na kumshikilia Njau katika Kituo cha Polisi Majengo kutokana na tuhuma za unajisi, lakini baadaye tulimwachia kwa dhamana. Upelelezi wa tukio hili utakapokamilika tutamfikisha mahakamani mtuhumiwa huyo," alisema.

Inadaiwa kuwa mwanafunzi huyo ambaye ni Mkazi wa Kitongoji cha Kikowonyi, Kijiji cha Mwasi Kusini, Wilaya ya Moshi, alianza kunajisiwa na mtuhumiwa huyo Januari mwaka huu.

Hata hivyo, mwanafunzi huyo anadai kuwa hakutoa taarifa za vitendo hivyo kutokana na vitisho alivyokuwa akipewa na mtuhumiwa kwamba akitoa siri hiyo, atamuua.

Akizungumzia tukio hilo, Helena Temba ambaye ni bibi anayeishi na mwanafunzi huyo, alisema aligundua mjukuu wake kubadilisha mwendo wa kutembea na kila alipomuuliza alikuwa akimwambia tumbo linamuuna.

"Mjukuu alikuwa hasemi tatizo linalomsibu hadi juzi alivyoamua kueleza ukweli, kwamba alikuwa akifanyiwa ukatili na jirani yangu, ambaye alikuwa rafiki wa mwanangu.

"Sasa baada ya kueleza hilo tatizo ilibidi tumpeleke hospitalini na alipofanyiwa uchunguzi wa kitabibu alikutwa ameingiliwa sehemu za siri na ameambukizwa magonjwa ya zinaa," alisimulia.

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kikowonyi, Magdalena Maro alikiri kuwa taarifa hizo ni kweli.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwasi Kusini, Omary Sinari adai kuwa pamoja na mtuhumiwa kukamatwa, amerejea mtaani na anaendelea na kujigamba baada ya kuachiwa kwa dhamana.



# Jumuiya ya Maridhiano yamtunuku Rais Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JUMUIYA ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma imetoa tuzo kwa Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kuutambua mchango wake mkubwa katika kuiongoza Tanzania kwa amani.

Tuzo hiyo ilipokewa na Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule kwa niaba ya Rais Samia wakati wa mkutano mkuu maalum wa kuombea nchi uliofanyika jijini hapa juzi.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Askofu Dk. Evence Chande alisema pamoja na kumpa tuzo Rais, pia wametoa kwa Mkuu wa Mkoa na wakuu wa wilaya za Dodoma kutokana na kutambua mchango wao mkubwa wa kuwatumikia watanzania na kuifanya nchi kuendelea kuwa na amani.

"Sisi Jumuiya ya Maridhiano Tanzania Mkoa wa Dodoma tunaihakikishia serikali kuwa tutadumisha amani na kutoa elimu kupitia madhehebu ya dini tunazoabudu ili watanzania waipende nchi yao na viongozi wao," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary, alisema serikali inatambua na kutegemea jumuiya hiyo kuhubiri amani kwa waumini wao kupitia madhehebu yao.

Alisema serikali itaendelea kuzitatua kero mbalimbali zinazowakosesha amani wananchi.

Aliwahimiza watanzania kuendelea kuwapenda na kuwaamini viongozi wao ili kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

# Utafiti wabaini idadi ndogo wanawake shahada ya 2, 3

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, umebaini idadi ya wanafunzi wa kike ngazi ya elimu ya juu hupungua kwa kasi pindi wanapoanza kusoma shahada ya pili na tatu kutokana na majukumu ya kifamilia.

Kutokana na hali hiyo taasisi hiyo imeanza ujenzi wa bweni maalum kwa ajili ya wanachuo wanawake wenye mahitaji maalum na wenye watoto wadogo.

Vilevile, taasisi hiyo ipo kwenye hatua za mwisho kuingiza sokoni mfumo wa kubaini machapisho ya wizi kwa kuwa unaotumika katika vyuo vingi nchini ni wa kutoka nje na wa gharama kubwa.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari jijini hapa, Makamu Mkuu wa Taasisi hiyo, Prof. Emmanuel Luoga alisema: "Ukiangalia idadi ya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari utakuta wavulana na wasichana ni 50 kwa 50, lakini tunavyozidi kwenda juu idadi ya wanawake inapungua sana kulinganishwa na wanaume."

Alibainisha kuwa hali hiyo inatokana na wanawake kuanza kujihusisha na masuala ya familia, utafiti wao ukibaini wanapofikia hatua ya kusoma shahada ya pili au tatu huanza kulea.

"Mazingira ya vyuo vyetu vingi siyo wezeshi kusaidia wanawake wa namna hii, tulitoa ombi maalum la kupata mabweni ya kinamama wenye watoto wadogo na mahitaji maalum ambapo serikali ilitoa fedha na kibali cha kujenga jengo hilo," alisema.

Alibainisha kuwa ujenzi uliananza Oktoba 2021 na sasa umefikia asilimia 43 na utafanyika kwa awamu tatu, ambapo awamu ya kwanza itachukua wanafunzi 180, ukikadiriwa kutumia Sh. bilioni 4.8 na utakamilika Juni 2023.

Prof. Luoga alisema mradi huo utachochea mapinduzi ya elimu na utafiti hasa kwa wanawake.

Akizungumzia vipaumbele vingine, Makamu Mkuu wa Chuo hicho alisema taasisi inajikita katika matumizi ya TEHAMA ambapo itapata dola za Marekani milioni 10, mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia ili kuimarisha mifumo ya TEHAMA na kuhakikisha wanapata ithibati ya maabara yao kufikia viwango vya kimataifa.

Pia alisema taasisi hiyo itashirikiana na taasisi zingine mbili, wakitarajia kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Ndizi ambacho kitahusika na masuala ya utafiti wa mbegu, namna ya kuongeza tija katika upandaji na usimamizi wa zao la ndizi na matumizi bora.

"Taasisi inafanya utafiti mwingi wa kuzalisha viuatilifu asilia ili kupambana na magonjwa ya mimea, hivyo kuongeza tija katika kilimo. Pia tumeendelea kubuni majiko sanifu yanayopunguza gharama ambayo yanatumia gesi na nishati zingine mbadala," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa alisema serikali inafanya kazi kubwa kuandaa wanasayansi kutoka shule za msingi mpaka shahada za kwanza ambapo kwa sasa inajenga shule moja ya sekondari ya masomo ya sayansi kwa kila mkoa kwa ajili ya wasichana.



Mama mchuuzi vikapu, kofia na fagio, akisaka wateja wa bidhaa zake katika eneo la kituo cha daladala cha Sabasaba, jijini Dodoma jana. Kikapu kimoja alikiuza kwa bei ya 3,000/-, kofia 2, 500/- na fagio 1,500/-. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Majadiliano yaokoa mabilioni ya serikali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali imeokoa Sh. bilioni 6.65 kutoka kampuni moja ya mawasiliano nchini baada ya kukamilisha majadiliano ya mgogoro kati yake na serikali.

Vilevile, ofisi hiyo imepunguza idadi ya migogoro dhidi ya serikali iliyofunguliwa kwenye mahakama na mabaraza nje na ndani ya nchi.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Boniphace Luhende alibainisha hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Luhende alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuvutia wawekezaji nchini kwa kumaliza migogoro mbalimbali dhidi ya wawekezaji na wafanyabiashara kwa njia ya majadiliano.

"Mashauri ya kampuni ya moja ya mawasiliano nchini ambapo mnamo Juni 10, 2021, ofisi ilikamilisha majadiliano yaliyoingizia serikali kiasi cha Sh. bilioni 6.645. Fedha hizi zililipwa TAMISEMI," alisema. Alitaja shauri lingine ni la usuluhishi baina ya G.S Engineering &Construction Corporation (South Korea) dhidi ya Wakala wa Barabara (TANROADS).

Pia alisema shauri la usuluhishi wa kimataifa kati ya Kampuni ya Heritage Rukwa (Tz) Limited dhidi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli la Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mgogoro baina ya M/s SMEC International dhidi ya REA pamoja na mashauri mengine mengi.

"Agizo la Rais limesaidia kupunguza idadi ya migogoro dhidi ya serikali iliyofunguliwa kwenye mahakama na mabaraza nje na ndani ya nchini, kuokoa fedha za serikali ambazo zingetumika katika kuendesha migogoro tajwa, kudumisha uhusiano kati ya serikali na wawekezaji," alisema.

Pia alisema kujenga imani kwa wawekezaji kuhusu hali ya utoaji haki nchini pamoja na kukuza diplomasia ya uchumi.

Kiongozi huyo pia alibainisha kuwa kwa kipindi cha miaka minne, ofisi hiyo imekuwa ikiiwakilisha serikali mahakamani na katika mabaraza ya usuluhishi ambapo imeendesha mashauri 6,043. Kati yake, ya madai ni 5885 na ya usuluhishi 158.

"Mashauri ya madai yaliyomalizika katika kipindi cha miaka minne upande wa madai ni 582 na ya usuluhishi ni 60. Kati ya hayo, serikali imeshinda mashauri 530 ya madai na mashauri ya usuluhishi 31," alisema.

Pamoja na mafanikio hayo, alisema ofisi imeanzisha mfumo imara wa Tehama uitwao CIMS unaosajili mashauri mbalimbali yanayoendeshwa.





## Wakulima wa mwani waanza kupokea boti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZAIDI ya wakulima 1,500 wa mwani wameanza kupokea mgawo wa boti kwa ajili ya kilimo hicho ambacho kinalimwa na wanawake kwa asilimia 80 pamoja na vifaa vyake ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa uchumi wa buluu.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Suleiman Makame, aliposhiriki katika mgawo wa boti za wakulima wa mwani pamoja na vifaa vya kilimo hicho, Kojani na Wete kisiwani Pemba.

Alisema, mikakati ya serikali ni kulifanya zao la mwani kuwa la biashara zaidi, hivyo wakulima wake sasa wanatakiwa kulima kwa kutumia mbinu za kisasa za kitaalamu.

Waziri alisema katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya uchumi wa bluu, serikali ya Zanzibar imetenga Sh. bilioni 36 ambazo zitawawezesha wananchi kupiga hatua kubwa katika mageuzi ya uchumi wa bluu.

Aidha, alisema katika fedha hizo, boti 500 zitatengenezwa kwa ajili ya wakulima wa mwani, kilimo ambacho kwa sasa kinakabiliwa na mageuzi makubwa yakiwamo mabadiliko ya tabianchi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya nane kipaumbele chake ni uchumi wa bluu na kuona wananchi wananufaika na rasilimali za baharini ikiwamo mwani ambacho kwa asilimia 80 kinalimwa na wanawake," alisema.

Alisema Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu inaendelea na kazi za utengenezaji wa mabwawa 100 ambayo yatatumika kwa kazi za ufugaji wa samaki ikiwamo majongoo ya bahari.

# Wataka sheria mtoto irekebishwe kupunguza ukatili dhidi ya watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya Sheria ya Mtoto Zanzibar ya mwaka 2011 kupata tunzo ya kimataifa, wadau wa kupinga vitendo vya udhalilishaji wametaka ifanyiwe marekebisho.

Tuzo hiyo ilitolewa mjini Geneva, Uswisi na Shirika la World Future Council pamoja na Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) mwaka 2015.

Wakizungumza jana katika kikao cha uwasilishaji wa taarifa za takwimu za udhalilishaji za Septemba, mwaka huu, walisema kitendo cha watoto wanaoshtakiwa na vitendo vya udhalilishaji kutopewa adhabu kali kumesababisha uwapo wa kesi nyingi zinazowahusu watoto walio chini ya umri wa miaka 18.

Kikao hicho kilichofanyika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, wadau hao walisema watoto wanaokinzana na sheria kwa kushtakiwa kujihusisha na vitendo vya udhalilishaji, adhabu zao hupelekwa katika vituo vya kurekebisha tabia.

Mwenyekiti wa Mahakama ya Watoto Zanzibar, Zuena Muhammed Abdulkadir, alisema kutokuwapo kwa adhabu kali kwa watoto wanaokutwa na hatia kwa vitendo vya udhalilishaji kumesababisha kuwapo kwa udanganyifu wa kughushi vyeti vya kuzaliwa kwa watuhumiwa wa kesi hizo.

Mwenyekiti huyo alisema watuhumiwa hao wanafanya hivyo wakijua kuwa watoto walio chini ya miaka 18 hawapewi adhabu kali na badala yake hupewa onyo, faini au kupelekwa katika kituo cha kurekebisha tabia.

"Sheria ya Mtoto Zanzibar imeeleza kutomtia hatiani mtoto chini ya miaka 18 anaekutwa na hatia ya makosa ya udhalilishaji na badala yake kupelekwa katika kutuo cha kurekebisha sheria," alisema

Alisema ziko kesi za watoto waliojihusisha na vitendo vya ulawiti na ubakaji kwa watoto wenzao zaidi ya mara moja kwa sababu hakuna adhabu kali inayotolewa dhidi yao.

"Akikutwa na hatia ya udhalilishaji anapelekwa kituo cha kurekebisha sheria ambako katika kituo hicho mtoto anapewa hadi nauli ya kwenda na kurudi lakini cha kushangaza akimaliza adhabu yake huko anaenda tena kufanya vitendo vya udhalilishaji," alisema.

Akiwasilisha takwimu za udhalilishaji kwa mwezi wa Septemba, Ramla Hassan Pandu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, alisema kesi 170 zimeripotiwa na kati ya hizo, 152 waathirika ni watoto na 18 wanawake.

Ramla alisema katika kesi hizo 77 ni za kubaka, 32 kulawiti, 14 kuingilia kinyume cha maumbile, 12 kutorosha, 12 shambulio la aibu au kukashifu na 23 shambulio.

Alisema, idadi ya matukio hayo 170 yameongezeka kutoka matukio 131 yaliyoripotiwa Agosti, mwaka huu.

Pia, alisema Wilaya ya Magharibi B Unguja, inaongoza kwa matukio ya ubakaji ikilinganishwa na wilaya zingine ambapo matukio ya kubaka 24 kati ya matukio yote 77 ya kubaka yametokea wilayani humo.

Aidha, alisema matukio 125 kati ya matukio 170 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa polisi, 39 yapo katika ofisi ya mkurugenzi wa mashtaka na matukio sita yako mahakamani.

Halima Abdulrahman Omar, Mkuu wa Kitengo cha Jinsia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, alisema hali kwa sasa ni mbaya, hivyo lazima kuchukua hatua madhubuti kuwalinda watoto.

Said Ali Said, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi kutoka kitengo cha takwimu makao makuu ya polisi Zanzibar, alisema lazima jamii kuwa wawazi kueleza madhara ya udhalilishaji kwa watoto kwa sasabu wahalifu wanambinu tofauti katika kufanya vitendo hivyo.

Alisema licha ya adhabu kali zinazotolewa lakini vitendo vinaendelea kwa wingi na watoto wanaokidhana nasheria adhabu zilizopo hazimuathiri.



Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kizimkazi, wakati wa ziara zake za kusikiliza kero za wananchi kisiwani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamlaka yavunja rekodi ya mapato

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) imevunja rikodi ya ukusanyaji wa mapato baada ya kukusanya Sh. billioni 6,778,716,329.97 katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu. Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 96 kulinganisha na mwaka jana.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Seif Abdallah Juma, alisema ongezeko hilo linatokana na jitihada zilizofanywa na Rais Dk. Hussein Mwinyi kuipatia wataalamu waliobobea katika usimamizi na uendeshaji wa viwanja vya ndege duniani kutoka kampuni ya SEGAP ya Ufaransa.

Alisema mamlaka hiyo pia imepokea wageni 553,592 waliofikia Zanzibar kwa kutumia usafiri wa anga ambao wameingiza Sh. 2,759,819,288.03 tokea mwaka 2013 iliponza rasmi shughuli zake kutoka iliyokuwa idara ya usafiri wa anga.

Makusanyo haya, alisema ni matokeo ya kufanikiwa kwa kiasi kikubwa filamu ya Royal Tour iliyoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ambayo imefungua fursa na ongezeko la watalii kufika nchini pamoja na ongezeko kubwa la maombi ya mashirika ya ndege ya kimataifa kufanya safari katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA) ambao ni moja ya vyanzo muhimu vya mapato.

Pia, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 kipindi cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba, kabla ya kuanza kwa mdororo wa kiuchumi duniani uliosababishwa na maambukizi ya virusi vya Corona, mamlaka ilikusanya Sh. 2,988,220,807.98 pekee.

Alisema ongezeko hilo la mapato ni la kwanza kuwahi kufikiwa katika historia ya makusanyo ya mamlaka hivyo tunaipongeza serikali kwa jitihada mbalimbali inayoendelea kuzichukua kwa nia ya kuimarisha mapato yanayotokana na usafiri wa anga nchini.



## SHAKIRA
UKURASA 18





# JOKATE

UKURASA WA 15

YUKO WAPI ?

# SALUM ABDALLAH-2

## Kutoka familia tajiri hadi mwanamuziki maarufu



**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tulianza makala ya mwanamuziki maarufu kuwahi kutokea kwenye ardhi ya Tanzania, Salum Abdallah Yazidu (SAY).

Ndiye anayetajwa kuwa ni mmoja wakati wa wanamuziki wachache walioanza kuweka msingi ya wanamuziki wengi waliokuja kuwa nyota baadaye, akiwamo Mbaraka Mwingine, Juma Kilaza na wengine ambao wamepitia mikononi mwake.

Tulianza kuangalia maisha yake tangu alivyozaliwa Mei 5, 1928 na kulelewa kwenye mazingira ya kitajiri, lakini alivyoanza kuupenda muziki kiasi cha kukorofishana mara kwa mara na baba yake, ingawa alisalimu amri kwa kumnunulia 'rekodi pleya' ili awe anatulia dukani, lakini alipotimiza miaka 15 baba yake alianza kumtuma kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya kununua bidhaa kwa ajili ya maduka na hoteli zake. Leo inaingia kwenye hatua ya pili.

Mahudhurio ya mara kwa mara kwenye bendi hiyo na zingine kidogo, yalizidi kumpagawisha na kumfanya akili yake iwe kwenye muziki zaidi ya kitu chochote kile.

Miaka michache baadaye, aliuza moja kati ya nyumba nyingi za baba yake kwa siri na kununua vyombo vya muziki, na hapo tayari alishaanza kuwa na ufahamu na ujuzi wa muziki.

Akiwa nyumbani alianza kuwafundisha baadhi ya wafanyakazi wa hoteli za baba yake muziki.

Na hao ndiyo waliokuwa wanamuziki wake wa kwanza kwenye bendi yake aliyoiita La Paloma, iliyokuwa na vyombo baridi ambavyo si vya umeme mwaka 1948, akiwa na miaka 20 tu.

Neno La Paloma, lilitokana lilikuwa ni jina la wimbo maarufu ambao uliotoka Cuba ukiwa na jina hilo lenye maana Njiwa.

**Zengwe la rafiki za baba yake**

Bendi hiyo ilikuwa ikipiga muziki kwenye sherehe na hafla mbalimbali za kijamii kama vile harusi na mingine, mikutano ya kudai uhuru, na mara nyingi ilikuwa ni siku za wikiendi.

Baadhi ya wafanyakazi wa mahoteli ya kina Salum ambao tayari walishafuzu kwenye muziki, walikuwa wakifanya kazi mchana, lakini usiku wanakwenda kupiga muziki wikiendi, huku siku za kawaida wakiwa wanafanya mazoezi.

**Kama nilivyosema huko juu, wakati huo bado muziki ulichukuliwa si tu ni kazi ya watoto wa masikini, lakini pia ni uhuni, lakini mzee Abdallah alikuwa ndiyo kama mwenyekiti wa wazee wa Kiarabu Morogoro, hivyo ilionekana kama anawadhalilisha, pia kuidhalilisha itikadi yao.**

Hata hivyo, kitendo hicho kiliwakera baadhi ya marafiki wa mzee Abdallah na kumwambia waziwazi kuwa mtu mwenye heshima zake kama yeye, tajiri, muungwana, pia mwenye itikadi safi, haiwezekani mtoto wake apige muziki.

Kama nilivyosema huko juu, wakati huo bado muziki ulichukuliwa si tu ni kazi ya watoto wa masikini, lakini pia ni uhuni, lakini mzee Abdallah alikuwa ndiyo kama mwenyekiti wa wazee wa Kiarabu Morogoro, hivyo ilionekana kama anawadhalilisha, pia kuidhalilisha itikadi yao.

Baba yake hakujua la kufanya, kwa sababu yaliyosemwa na rafiki zake aliyaona ni kweli, pia alimpenda kijana wake na hakutaka kumkera kwa sababu alionekana kuwa na akili ya kusimamia mali nyingi zake.

**Atoroka na kuzamia meli**

Maneno na zengwe lile lilimfikia mwenyewe Salum. Akaamua aondoke mjini Morogoro. Na si Morogoro tu, bali nchini.

Alitaka kuondoka kwa sababu mbili. Kwanza kabisa ni kuondokana na zengwe na maneno ambayo yalimfanya asifanye kazi yake ya muziki kwa raha. Lakini bado alijiona hajawa na uwezo mkubwa wa kimuziki, hivyo aliamua kwenda nchini Cuba kujifunza muziki zaidi.

Hata hivyo, kutokana na hali ya kisiasa wakati huo duniani kutokana na mgogoro wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, meli aliyozamia, ilishindwa kwenda Cuba na kuishia Mombasa nchini Kenya, ikisikilizia usalama kwanza.

Ilibidi Salum akae Mombasa kwa muda mrefu na pesa za kujikimu zilipokwisha, ilibidi aanze kazi ya kuuza mishikaki mitaani.

Siku moja akiwa kwenye matembezi alikuta sherehe za maulidi kwenye nyumba moja na vijana walikuwa wakipiga dufu na kughani.

Alipendezwa mno, hivyo naye alijiunga nao. Naye alianza kughani kwa sauti ilimshtua kila mtu, kiasi kwamba kila mmoja alitaka kumfahamu yeye ni nani na anaishi wapi.

Ingawa hakutaka kujitambulisha sana, lakini baadhi ya Waarabu wafanyabiashara kati ya Mombasa, Dar es Salaam na Morogoro walimtambua kuwa ni Salum, mtoto wa mzee Abdallah Yazid wa Morogoro.

Na baadhi walikuwa ameshapata taarifa za kupotea kwa kijana wa mzee Yazid mjini Morogoro na hajulikani alipo.

Vyama vya kusaidiana vilikuwapo tangu zamani, hivyo wanachama wa Chama cha Waarabu Afrika Mashariki ambacho pia mzee Abdallah Yazid ni mwanachama wake, walichanga pesa na kuamua kumsafirisha kutoka Mombasa hadi Morogoro.

**Itaendelea wiki inayokuja**



# WAKATI WOWOTE KUITWA MAMA

NI wazi kuwa, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, mkoani Dare s Salaam Jokate Mwegelo, wakati wowote anaweza kuwapa zawadi ya mtoto kichanga kama zawadi ya kumaliza mwaka 2022.

Jokate ambaye pia ni mwanamitindo, amewashtukiza watu kupitia ukurasa wake wa Instagram baada ya kuweka video fupi akionekana akiwa kavalia gauni pana, huku ujauzito wake ukionekana dhahiri.

Hata hivyo, baadhi ya wafuasi wake walioshiriki kuweka ujumbe katika posti hiyo, walielezea hisia zao tofauti huku wengine wakimpongeza kwa kutarajia kupata mtoto hivi karibuni.

Kiongozi huyo anakuwa wa kwanza kama mkuu wa Wilaya kuonekana akichapa kazi muda wote akiwa mjamzito, kiasi ambacho Watemeke wamembatiza jina la 'Mwanamke wa Shoka'.

Wafuasi wake wamempongeza kwa ujasiri wake na kwamba wanamuombea kwa Mungu kumpokea mtoto wake wa kwanza kwa hali ya furaha. Hawa ni baadhi ya watu waliojitokeza kutoa maoni yao katika video hiyo.

Mtu anayejiita HYPERLINK "https://www.instagram.com/lawrence_matemu/" lawrence_matemu ameandika "Karibu kwenye chama letu la wazazi mdogo wangu, sasa umekua haswaa na Mungu akujalie uzao salama kwa jina la Yesu Kristu mwana wa Mungu aliye hai"

Mwingine HYPERLINK "https://www.instagram.com/drsamofficialtz/" drsamofficialtz ameandika "Dc wetu tunakupenda sana siku moja naamin utakuwa raisi" na kisha

HYPERLINK "https://www.instagram.com/mamap_beauty_saloon/" mamap_beauty_saloon "Nakupenda sana mwanamke wa shoka"

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**





**@billnass**
Warumi 12 :
Kwa hiyo ndugu zangu nawasihi kwa sababu ya huruma zake Mungu, jitoeni kwake muwe sadaka hai, takatifu na inayompendeza Mungu, ambaye ndio ibada yenu ya kiroho. 2 Msiige tabia na mienendo ya dunia hii bali mbadilishwe, nia zenu zikifanywa kuwa mpya, ili mpate kuwa na hakika ni nini mapenzi ya Mungu: yaliyo mema, yanayopendeza machoni pake na makamilifu.

**@officiallinnah**
Moyo umekubali wewe unyanyasike, umridhishe mtu





**@esha.s.buheti**
Wabongo shikamooooo uwiii leo nimetagiwa sana, kuna page imepost watu watag wapishi wao wanaowakubali basi kuna comment nyingine nimeona nimetagiwa na baadhi ya wapishi wenzangu nikasema ngoja nifungue nione wanavyopika. Heee si nakuta nimeblokiwa na hizo akaunti za wapishi, ni uoga au ni nini? na hali hiyo sijaanza kununua tuzo, nikianza na mimi si mtanipiga mawe hebu tufanyeni kazi acheni kukunja nafsi riziki zinatoka kwa mungu.

**@shamsaford**
Unapofikilia kunifanyia mabaya au kuniangusha kumbuka nyuma yangu kuna watu wanaonitegemea mimi ndo mboni yao





**@batuliactresstz**
Kipaji Kinapokutana na Juhudi@Ramadhanibrothers hongereni

BASI SAWA

## BSS yaanza kwa mbwembwe




WATANZANIA wataanza kushuhudia hivi karibuni burudani tamu kutoka shindano la kuibua vipaji vya muziki la Bongo Star Search.

Akiongea na wanahabari muasisi wa shindano hilo, Madam Rita amesema mwaka huu litakuwa tofauti baada ya kuyapatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zilizojitokeza mwaka jana.

Ameongeza kuwa msimu wa 13 wa BSS, kuna mabadiliko mengi kuanzia wakati wa kuwatafuta washiriki na ndani ya nyumba ambayo washiriki wataishi kwa ajili ya kumtafuta mshindi.


## Town Classic kuzinduliwa Novemba



BENDI mpya ya muziki wa dansi ya Town Classic imeshuti video ya wimbo mmoja uliopewa jina la 'No Stress' ambao kipande cha video yake kimerushwa kwenye mitandao ya kijamii.

Meneja wa bendi hiyo Andrew Sekidia, ambaye pia ni mpiga kinanda, amesema kionjo hicho ni utambulisho wa ujio wa bendi hiyo ambayo itazinduliwa rasmi mwishoni mwa mwezi ujao.

Sekidi amesema bendi hiyo pia ina wimbo mwingine uitwao 'Shem Darling' ambao utajumuishwa katika nyimbo zitakazotumbuiza siku ya uzinduzi.



# NANI KAWALOGA MASTAA BONGO?

BAADA ya mke wa Mwimbaji wa Bongo Fleva, Alikiba aitwae Amina kuweka ishara ya kuwa ndoa yake imekwisha, kumeibua mjadala mkali mitandaoni.

Watu wengi wanahoji kwa nini mastaa wengi hawadumu katika ndoa zao, na kueleza labda maisha ya anasa yanayowazunguka yanasababisha kutoheshimu ndoa zao.

Hivi karibuni Amina aliandika kwenye insta habari yake kwa herufi kubwa "OFFICIALLY FREE" akimaanisha sasa ni rasmi yuko huru.

Hata hivyo, mjadala ulizidi kupamba moto baada ya baadhi kuorodhesha mastaa wengine ambao ndoa zao zilianguka ghafla na kuwataka wengine waliongia katika maisha hayo kuwa makini na kujifunza kwa wenzao.



# Basata yataka yaishe Konde Gang

UTATA wa hatma ya kutimuliwa kwa wasanii Cheed na Killy katika lebo la Konde Gang, unazidi kutanda baada ya Baraza la Sanaa Tanzania, kueleza vyombo vya habari vinapotosha mgogoro huo.

Kupitia XXL ya Clouds Fm, Ofisa sanaa mwandamizi wa Baraza la sanaa Tanzania (BASATA), Abel Ndaga amesema kila kitu kitakwenda vyema na kwamba kinachoangaliwa ni namna ya pande hizo mbili kuwa sawa.

Ndaga, amesema lengo la BASATA ni kuendeleza tasnia ya sanaa nchini na kwamba kunapozuka sintofahamu ina wajibu wa kuingilia kati kusuluhisha.

"Katika mgogoro huu wasanii hawa walipoleta malalamiko, tuliyapokea lakini siku ya kwanza Konde Gang hawakufika kikaoni, siku ya pili wakatuma mwakilishi na baada ya majadiliano na mwakilishi, wao kama Konde Gang walihitaji siku mbili mbele ili waweke mambo yote sawa na yote inatokana kutafuta suluhu," amesema Ndaga.

# BENDI 5 ZA VERCKYS ZILIZOTIKISA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

MASHABIKI wa muziki wa dansi Afrika na dunia kwa ujumla walipatwa mshtuko Oktoba 13 walipotangaziwa kifo cha mwanamuziki, mtunzi, kiongozi wa bendi, mtayarishaji muziki na mfanyabiashara, Kiamuangana Mateta maarufu kama Verckys aliyefariki kwenye jiji la Kinshasa nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Mwanamuziki huyo ambaye sifa yake kubwa iliyompatia umaarufu ni kupiga ala ya upepo kwenye muziki inayoitwa saxophone, alifariki akiwa na umri wa miaka 78. Alijifunza muziki kanisani.

Alimpenda sana mpiga saxophone maarufu sana wa Kimarekani wakati huo King Curtis, akawa anaiga upigaji wake hadi akaanza kujiita jina la mwanamuziki huyo.

Kutokana na matamshi ya Kifaransa jina 'Curtis' yeye alikuwa akisikia kama likitamkwa 'Verckys' na ndiyo mwanzo wa kujiita hivyo.

Hata hivyo, kutokana na kumiliki bendi nyingi kwa njia moja ama nyingine, mashabiki wake wakampachika jina la 'Wazolambongo' yaani mzoa pesa, kutokana na kuwa mwanamuziki, mmiliki wa bendi kadhaa na kufungua studio za kurekodi santuri kiasi cha kumuingizia pesa nyingi.

Historia nzima ya mwanamuziki huyo utaisoma kesho kikamilifu kwenye gazeti na Nipashe Jumapili, lakini leo tuangalia bendi tano zilizokuwa chini yake ambazo zilitoa nyimbo ambazo zilikuwa maarufu sana hapa nchini.

### Orchestra Veve

Hii ndiyo bendi aliyekuwa akiimiliki kwa asilimia 100 Verckys na neno Veve ni kifupi cha jina lake hilo, akichukua herufi za mwanzo Ve mara mbili na kuwa jina la bendi ambayo yeye mwenyewe alikuwa akiipigia ambapo alifanya balaa sana kwenye saxophone.

Ilitamba na nyimbo kama 'Baruti', 'Kalala', 'Bilobela', 'Muana Mburu', 'Mikolo Mileki Mingi' na 'Lukani', zilizotamba sana nchini mwanzoni mwa miaka ya 1970.

### Orchestra Bella Bella

Pamoja na kuwa ilikuwa ikiongozwa na Soki Vangu, lakini bendi hii pia ilikuwa chini ya Verckys kwa sababu ndiye aliyekuwa akiifadhili kwa kuipa vyombo na kuwarekodia nyimbo zao kwenye studio yake kiasi cha kuifanya kujulikana na kuwa bendi tishio nchini Zaire (sasa Congo). Baadhi ya waimbaji wa bendi hii ni Pepe Kalle na Nyboma Mwandido.

### Orchestra Lipua Lipua

Ilikuwa bendi maarufu nchini Zaire wakati huo na Afrika Mashariki na Kati ikiwa na vibao kama 'Mombasa', 'Mbondo', 'Mfueni', 'Matoba' na nyingine nyingi zilizotamba sana nchini Tanzania. Nayo ilikuwa chini ya Kiamuangana 'Wazolambongo' Mateta Verckys. Bendi hii ilikuwa ni zao la bendi ya Bella Bella ambayo iligawanyika, Soki Vangu akaondoka na jina kwenda kuunda Bella Bella nyingine, na waliobaki kina Pepe Kalle wakabadili jina kujiita Lipua Lipua. Lakini zote hizi zilibaki chini ya usimamizi na ufadhili wa Verckys.

### Orchestra Kiam

Kama kawaida, Verckys alikusanya vijana wengine na kutengeneza bendi iliyoitwa Orchestra Kiam, neno hilo likiwa ni kifupi cha jina lake Kiamuangana.

Nyimbo zake zilizonyanyasa sana nchini ni 'Moni Afinda', 'Kamiki', 'Mbale', Memi na nyinginezo.

### Orchestra Les Kamale

Asossa na Nyboma walijiondoa Lipua Lipua wakaenda kuunda bendi nyingine Les Kamale, Pepe Kalle yeye akaenda kuunda Empire Bakuba.



Bendi hizi zote nazo zilikuwa chini ya usimamizi wa Verckys, akizifadhili kwa kurekodi na vyombo, ingawa baadaye Empire Bakuba ya Pepe Kalle iliweza kusimama yenyewe na kujiondoa, lakini Les Kamale iliendelea kuwa chini ya marehemu hadi ilipovunjika mwanzoni mwa miaka ya 1980.

FILAMU

# My in Law: Mama mkwe kizabizabina

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU inaitwa 'My in Law', inayoonyesha baadhi ya matatizo yaliyomo kwenye baadhi ya familia zetu za Kiafrika.

Lakini kwa siku za karibuni tumegundua kuwa baadhi ya matatizo au changamoto tunazoziona kwenye ukoo au familia za Kiafrika zipo pia kwenye tamthilia za Kihindi, Kihispania, Kifilipino na nyinginezo, hivyo kuonyesha baadhi ya mambo hayo yanafanana tu.

Kwenye filamu hii tunamuona mama mmoja mwenye roho mbaya, ya kwa nini, chuki, muongo na kizabizabina.

Mama huyu tangu kijana wake aoe alikuwa akifanya kazi ya kumtesa 'mka mwana' wake licha ya maonyo ya hapa na pale hadi kufikia kusababisha umauti.

Imechezwa na Mama Besenga, Roney, Dora, Chriss, Filipo na wengineo. Kijana Roney anaishi vema na mkewe Dora. Wanapendana kama chanda na pete, na kufuatana kama kumbikumbi. Mama mkwe anaonekana hapendezwi na tabia hiyo. Anaona kama vile mtoto wake amewekewa dawa ya mapenzi, maarufu kama 'limbwata.'

Huyu mama mkwe ana hila ya kwapa. Kila anachonunuliwa mkwewe na kijana wake, na yeye anataka anunuliwe.

Kuna siku kijana kamnunulia mkewe maua, akakasirika na kusema mbona yeye tangu amzae hajawahi kumletea maua. Alichofanya ni kumpora mkwewe na kuyachukua yeye.

Binti akavumilia mwisho akachoka na kumwambia mumewe achukue hatua ya kukomesha hali hiyo, vinginevyo anaweza kuondoka.

Kijana akamkanya mama yake juu ya tabia hiyo, lakini mwenye hila hana dawa, akaendelea.

Hata mwanaye akiwa amelala na mkewe, yeye alfajiri dirishani kwenda kumuamsha afagie, na maneno juu analala kitu gani wakati kumekucha.

Mama mzazi wa binti huyo akaja kumtembelea. Binti akafunguka madhila yote anayofanyiwa na mama mkwe wake, hadi wakati mwingine kufikia hatua ya kupigwa kama ngoma.

Mama wa binti huyo kumbe naye yupo vizuri kwa 'mineno' ya shombo. Akawapakia kijana huyo mpaka mama yake. Mama mkwe mwenyewe alipoa kama maji ya mtungini kwa timbwili alilofanya mama wa binti huyo.

Akapiga 'biti' kuwa anaondoka, akisikia binti yake amepatwa matatizo, basi watamjua yeye ni nani.

Ilibidi kijana aende kwa mama mkwe wake kuomba radhi kwa yote yaliyotokea na kuahidi hayatajitokeza tena.

Mama mkwe akamwambia kijana aondoke nyumbani pale kwani anakaa pamoja na mama yake ndiyo sababu. Akiondoka anaishi vema na mkewe Dora.



Kijana akataka kufanya hivyo kwani kampuni ilimpa nyumba, lakini mama yake aling'ang'ania kuwa kama anaenda kuishi huko na yeye anakwenda, na nyumba hiyo wapangishe.

La kuvunda halina ubani, mama mkwe aliendelea na tabia ya kumtesa dora. Siku isiyo na jina wakati Dora mjamzito alimfuata ndani na kumwambia ni mvivu hafanyi kazi yoyote zaidi ya kulala, akaanza kumpiga ngumi za tumboni ambayo zilimpeleka chini na kuzirai.

Wakati anafanya kitendo hicho Roney aliwasili nyumbani gahfla na kukuta tukio hilo la kinyama. Alichukua bastola na kumtwanga mama yake kichwani naye akaanguka chini. Alipokwenda kuwakagua wote wawili walikuwa wameshakata roho.

BARIZI LA PWANI

# SHAKIRA SAID-3

# Mwimbaji mkongwe wa taarab, Mwenye sauti tamu ya kinanda



KATIKA mwendelezo wa makala inayomuhusu mwimbaji mkongwe wa Taarab nchini, Tatu Said maarufu kama Shakira, tumeona jinsi alivyoingia katika muziki huo na kuanza kupata jina.

Katika harakati ya kutafuta jukwaa la uimbaji, aliangukia katika kundi la Black Stars la mkoani Tanga, hapo alifanya maajabu kiasi ambacho jina lake lilipaa katika anga la Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Wiki hii tutaona jinsi Shakira Said alivyotumika kikamilifu katika siasa za nchini.

Rais wa awamu ya kwanza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alivutiwa na uimbaji wa Tatu bint Said 'Shakila', kiasi ambacho alimwalika kutumbuiza katika baadhi ya mikutano ya hadhara kabla ya Mwalimu Nyerere kuhutubia.

Mwaka 1987, alishawishiwa na aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo Dk. Salim Ahmed Salim, na kada wa Chama Cha Mapinduzi, Moses Nnauye, kuhama Tanga na kwenda kuongoza kikundi cha taarabu cha Jeshi la Kujenga Taifa Makao Makuu jijini Dar es Salaam.

Akiwa na kundi hilo miaka 1980 na 1990, nyota yake ilizidi kung'ara na kuwa miongoni mwa wasanii wakubwa ndani ya Afrika Mashariki na Kati.

Akiwa na kundi hilo alifyatua wimbo wa 'Kitanda kukaa Pembeni' ambao alikiri kuwa alikuwa ukiupenda sana.

Shakila, aliwahi kutamka kuwa aliimba kibao hicho mwenyewe kikiwa na nia ya kuuliza swali hilo ili apatiwe jibu toka kwa wasanii wenzake.

"Niliimba kibao hicho nikiwa na nia ya kujibiwa swali langu, lakini cha kushangaza hadi leo hii, bado swali langu hilo halijajibiwa na mimi sijakata tamaa bado nasubiri jibu litakaloniridhisha…" alisema Shakila wakati wa uhai wake.

Akizungumzia uhalisi wa Taarab, alielezea wakati huo taarab haikuimbwa bali ilighaniwa, na ndiyo maana waimbaji wake walikuwa wanakaa kwenye viti na kwa nia ya kufikisha ujumbe.

**Itaendelea wiki ijayo**



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Waluguru Original**
Bendi hii inafanya shughuli zake mjini Morogoro, hutoa burudani kuanzia Alhamisi katika ukumbi wa Didi's Break Point Iringa Road, Ijumaa ndani ya ukumbi wa Kambarage SUA, Jumamosi wapo Terminal Pub Msamvu na Jumapili wapo eneo hilo, katika ukumbi wa F2 Florida.

**Kimokimo Band**
Kundi hili linaloongozwa na mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa inatoa burudani ya nguvu katika ukumbi wa Mariot uliopo eneo Extertanal, leo lipo ukumbi wa Florida.

**Twanga Pepeta**
Jana ilifanya vitu vyake katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, leo Jumamosi ni ndani ya ukumbi wa Tabata Hotel na Jumapili kama kawaida ni katika ukumbi wa Gwambina Lounge (zamani TTC Club Chang'ombe).

**Mjengoni Classic Band**
Bendi yenye maskani yake jijini Arusha, kila Ijumaa na Jumamosi huwa inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili ipo Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**FM Academia**
Bendi hii ambayo inajulikana pia kama Wana Ngwasuma, chini ya rais wake Patcho Mwamba, leo Jumamosi itatoa burudani ya nguvu katika ukumbi wa Mawasiliano Park uliopo Ubungo.

**HQ Band**
Jana Ijumaa na leo Jumamosi kundi hili linaloongozwa na mwimbaji Rama Pentagon, lipo ndani ya ukumbi wa Lion Garden Kibaha Picha ya Ndege ambapo pia watakuwepo waimbaji nyota, Ally Choki na Mwinjuma Muumin.

**Tukuyu Sound Band**
Bendi mpya inayoongozwa na vijana machachari, Kalala Junior na Papii Kocha, kila Jumapili kama kawaida yao humalizia wikiendi katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park Ubungo.

**Orchestra Sikinde Original**
Bendi hii inayoundwa na wanamuziki waliojitoa kutoka bendi ya Sikinde Ngoma ya Ukae, leo Jumamosi ipo katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Beach, kesho Jumapili itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Msondo Ngoma**
Leo Jumamosi bendi hii kongwe itatoa burudani katika ukumbi wa Kwetu Pazuri Mbezi kwa Msuguri, kesho Jumapili kama kawaida itamalizia wikiendi katika ukumbi wa Dar Safari uliopo eneo la Buza.

**Mambo Live Band**
Kila Ijumaa inafanya vitu vyake katika ukumbi wa The Crown Pub, kisha Jumamosi inakuwa ndani ya ukumbi wa Village Hotel.

**Maina Band**
Bendi hii chini ya kiongozi na mmiliki wake Liston Maina, huanza kutoa burudani Alhamisi katika ukumbi wa The Marz, Namanga, Ijumaa Regancy Park, Jumamosi External na Jumapili katika ukumbi wa Trinity Oysterbay.

# AKON NAYE KAFANYIWA



AWALI suala la kufanyiwa upasuaji wa kurekebisha viungo ulifanywa zaidi na mastaa Wanawake.

Wasanii hao wengi kutoka Ulaya, Marekani na wachache Afrika wamekuwa wakihangaika kila kukicha kutafuta matibabu hayo baada ya kuona sehemu ya kiungo chake hakiko sawa, hivyo wanataka kuwa kama wanavyoona wao.

Hata hivyo, Uturuki ni moja ya nchi zinazosifika kwa kufanya matibabu ya upasuaji wa kurekebisha viungo, kiasi ambacho kila mwaka wanapata idadi kubwa ya mastaa wanaokwenda huko kufanyiwa upasuaji.

Hivi karibuni staa wa muziki tokea nchini Marekani na mwenye asili ya Senegal, Akon ameweka rekodi ya kuwa miongoni mwa wasanii wachache wa kiume aliyeingia katika orodha ya waliofanyiwa upasuaji huo.

Akon, amekiri hivi karibuni kwamba alikwenda nchini Uturuki kwa ajili ya ufanyaji upasuaji wa kuotesha nywele na kuondoa kipara.

Kwenye mahojiano katika Podcast aliyofanya hivi karibuni na Bootleg Kev, Akon ameeleza kuwa ilimbidi kusafiri hadi nchini humo kuotesha nywele zake kutokana na kutopenda muonekano wa mwanzo.

Ameongeza kwamba kwa sasa anafurahia matokeo yake licha ya kukutana na maumivu makali wakati wa upasuaji.

Upasuaji huo umegharimu zaidi ya shilingi milioni 17 huku akidai ni pesa ndogo ukilinganisha na gharama za matibabu hayo nchini Marekani.

Msanii wa Marekani ambaye aliongoza kwa kufanyiwa upasuaji mara nyingi ni Michael Jackson, ambaye inasemekana alitumia kiasi kikubwa cha pesa kurekebisha mwonekano wa sura yake ikiwamo pua yake ambayo awali ilikuwa kubwa kimwonekano.


# Mercy kama kweli usiogope

MSHINDI wa Big Brother Nigeria, Mercy Eke amezungumzia madai kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na muuzaji magari mashuhuri IVD.

Mercy Eke, alienda kwenye mtandao wake wa kijamii kuzungumzia uvumi kwamba alikuwa na uhusiano na muuzaji magari mashuhuri IVD ambaye anatuhumiwa kumtesa mke wake hadi kupoteza maisha.

"Jina langu limechafuliwa kwa muda mrefu, hii ni mara ya kwanza na ya mwisho nazungumzia hili. Sababu ya mimi kuzungumzia uongo huu wa wazi," amesema.





## Black panther kuanzia Nigeria

Kampuni ya Walt Disney, kwa kushirikiana na Africa International Film Festival (AFRIFF) na FilmOne Entertainment, imetangaza rasmi kuwa Nigeria itaandaa onyesho la kwanza la Afrika la Black Panther inayojulikana kama Wakanda Forever.

Filamu inayotarajiwa kutolewa na Marvel Cinematic Universe italeta sura mpya ya ufalme wa Wakanda kuwa hai, yote hayo yatajulikana siku ya uzinduzi utakaofanyika huko Lagos mnamo Novemba, kabla ya kutolewa kwake katika sinema hadi Novemba 11.

Waanzilishi wenza wa FilmOne Entertainment, Moses Babatope na Kene Okwuosa, walielezea shauku yao kuhusu onyesho la kwanza la Filamu hiyo kwa Afrika Magharibi.

## Wizkid azidi kupaa

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Ayodeji Balogun, maarufu kama Wizkid, amevunja rekodi nyingine baada ya kuibuka namba moja kwenye jukwaa la utiririshaji nyimbo la kimataifa la Spotify.

Starboy ametangazwa kuwa msanii wa kwanza katika bara la Afrika na kuweka historia ya kutumia jumla ya wiki 100 kwenye Chati ya Albamu za Ulimwenguni za Billboard kupitia album yake ya 'Made in Lagos'ya kutazamwa zaidi kwenye mtandao huo wa Spotify.

Kulingana na data ya chati kupitia Spotify, mwimbaji huyo amefanikiwa kufikisha zaidi ya bilioni 5 kwenye Spotify.





## Kylie Jenner aogopa uzazi

MWANAMITINDO bilionea, Kylie Jenner, amesema anapambana kuuweka mwili wake sawa kutokana na kuongezeka uzito unaosababishwa na uzazi.

Kylie ambaye utajiri wake unatokana na bidhaa zake za vipodozi, amesema kuzaliwa kwa mtoto wake wa pili ambaye baba yake ni Travis Scott, ilimuongezea tatizo kiasi ambacho kilimfanya kuwa na hofu.

"Nililia bila kukoma siku nzima kwa muda wa wiki tatu za kwanza. Sikujua tatizo hili nitalikabili vipi kwa sababu naupenda mwili wangu," amesema wakati akishiriki katika kipindi cha maisha halisi katika televisheni.

## Guchi, Yemi wafurahia 'I Swear' ikilindima

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Guchi ameachia ngoma yake mpya iitwayo "I Swear", akiwa amemshirikisha mkongwe Yemi Alade .

Kazi hiyo ya kufa mtu imetayarishwa na mtayarishaji ChechDa, Guchi ameonyesha kuwa yeye ni malkia wa midundo ya mapenzi yaliyovunjika.

Muunganiko huu unaelezwa kuwa ni mkubwa katika muziki kwani umeweza kuleta radha ya tofauti katika muziki wa pop.



MAKALA

# Liz Truss:
# Mambo sita aliyopitia siku 45 madarakani

Na Mwandishi Wetu

HATIMAYE Waziri Mkuu wa Uingereza, Liz Truss amejiuzulu baada ya kukalia nafasi hiyo kwa siku 45 tu baada ya kushika nafasi hiyo.

Hata hivyo, Truss anavunja rekodi kwa kuwa Waziri Mkuu pekee nchini humo kukalia ofisi namba 10 kwa muda mfupi zaidi, baada ya mtangulizi wake Boris Johnson kufanya hivyo kutokana na shinikizo la wabunge.

Mrithi wake atachaguliwa katika uchaguzi wa ndani wa chama cha Tory,utakaofanyika wiki ijayo.

Wabunge wa Tory walimtaka Truss aondoke madarakani baada ya serikali yake kukumbwa na misukosuko ya kisiasa, kufuatia kupuuzwa kwa sera zake nyingi za kiuchumi.

**TRUSS ALICHAGULIWA NA WAJUMBE WA TORY SEPTEMBA.**

Katika hotuba yake, Truss alisema Chama cha Conservative kilimchagua kwa jukumu la kupunguza ushuru na kukuza ukuaji wa uchumi.

Lakini kutokana na hali hiyo, anatambua kwamba hawezi kutekeleza mamlaka ambayo alichaguliwa na Chama cha Conservative.

Hata hivyo, kiongozi huyo mwenye siasa zinazogeuka kila wakati, anaonekana ndani ya muda mfupi amekuwa wa kipekee kutokana na kukutana na mambo sita muhimu katika maisha yake.

Kuanzia mkutano wake wa kwanza na Malkia, hadi machafuko ya bajeti yake ndogo, wiki zake sita madarakani zimekuwa mchanganyiko wa nyakati za kihistoria na migogoro ya kisiasa aliyojiletea mwenyewe.

Hapa kuna matukio sita ya kukumbukwa kwa muda wake mfupi aliohudumu.



**MKUTANO WA KWANZA NA WA MWISHO NA MALKIA**

Ingawa ataingia kwenye historia kama waziri mkuu aliyekaa muda mfupi zaidi nchini Uingereza, Truss alipigwa picha kwenye picha ya mwisho ya hadhara na Malkia Elizabeth ll aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi nchini humo.

Siku mbili kabla ya kifo chake, Malkia alimwalika rasmi Truss kama waziri wake mkuu wa 15 na kuunda serikali.

Picha ya viongozi hao wakipeana mikono katika Kasri la Balmoral ilizua wasiwasi kuhusu afya ya Malkia, kwa sababu ya sura yake dhaifu.

Truss alinukuliwa akielezea kwamba anajisikia 'kuheshimiwa sana kukutana na Malkia katika moja ya matendo yake ya mwisho.

Kuporomoka kwa bajeti ndogo

Kwasi Kwarteng alitangaza bajeti ndogo, ikiwa ni pamoja na paundi bilioni 45 ya kupunguzwa kwa kodi, ambayo ilisababisha mtikisiko wa soko la hisa.

Truss alifanya kampeni juu ya mpango wa kupunguza ushuru na wiki kadhaa za muhula wake kama waziri mkuu, Kansela wake, Kwasi Kwarteng, alizindua mpango wa kupunguzwa kwa ushuru wenye thamani hiyo.

Lakini Kwarteng hakueleza jinsi punguzo hilo lingelipwa.

Bajeti ndogo ilitangazwa siku ya Ijumaa,lakini masoko ya hisa yalipofunguliwa tena Jumatatu iliyofuata asubuhi, pauni ilishuka hadi kufikia viwango vya chini dhidi ya dola.

Bajeti ndogo ilizua msukosuko wa soko, huku Benki ya Uingereza ikilazimika kuchukua makumi ya mabilioni ya pauni ili kuleta uthabiti wa mifuko ya fedha za malipo ya uzeeni, na viwango vya mikopo viliongezeka.

Waziri wa Fedha, alibatilisha baadhi ya mpango huo, lakini haikusaidia sana kuwatuliza wanasiasa katika chama cha Conservative.

Ingekuwa mpango wa kwanza wa kiuchumi kutangazwa na punde tu kuanza kubadilishwa, na kuwafanya wachambuzi wa uchumi kusema kwamba ulikuwa umekufa.

**MKUTANO MFUPI NA WAANDISHI WA HABARI**

Huku serikali ikiwa imetatizwa na mwitikio wa soko la hisa na uvumi mabadiliko makubwa, Kwarteng aliitwa kutoka kwenye mkutano wa kimataifa huko Washington DC siku moja kabla ya kukamilika, na akafutwa kazi.

Saa chache baada ya kufutwa kazi, Truss alikuwa na mkutano mfupi na waandishi wa habari ambapo aliulizwa mara kwa mara kuhusu uaminifu wake kama waziri mkuu.

Vipi mbona bado upo?, aliuliza mwandishi mmoja wa habari.

Ingawa alijibu maswali manne pekee, alijikwaa na majibu yake, akisisitiza kwamba alikuwa amechukua hatua ya kutuliza kuyumba kwa uchumi.

Utendaji wake usio wa kawaida wa dakika nane na waandishi habari haukuwashawishi Wabunge katika chama chake kwamba angeweza kuendelea kuwa kiongozi.

**JARIBIO LA MFALME CHARLES**

Kanda za video kutoka ndani ya hadhira ya kila wiki kati ya mfalme wa Uingereza na waziri mkuu ni nadra kutolewa.

Lakini picha zilipotolewa za Mfalme Charles lll akikutana na Truss kwa mara ya kwanza katika kasri la Buckingham, hazikusaidia sana kurejesha sifa yake kwa watu.

Alipokabiliwa na shinikizo kubwa kutoka kwa wabunge wenzake waliokasirika ndani ya chama, Mfalme alitumia mitandao ya kijamii kukasirika baada ya kumwambia Truss kama 'mpendwa au mpenzi' wakati wa mazungumzo yao.

Ingawa msemo huo unasemekana kuwa kama ishara ya maneno ya Mfalme, ubadilishanaji huo wa maneno wa sekunde 15 ulianza kuenea haraka.

Hivi karibuni baadhi walidhani kwamba mfalme alikuwa akitoa ufafanuzi kuhusu uongozi wa Truss, lakini vyanzo baadaye vilimwambia Mhariri wa Siasa wa BBC Chris Mason kwamba alikuwa akionyesha tu kusikitikia ratiba ya waziri mkuu, ambayo ilimwona akitembelea ikulu mara mbili katika kipindi cha saa.

**BARUA YA MAUDHI YA BRAVERMAN**

Siku moja kabla ya kuwasilisha barua yake ya kujiuzulu, Truss alipokea barua moja kutoka kwa Waziri wake wa Mambo ya Ndani, Suella Braverman.

Aliyekuwa mpinzani wa waziri mkuu, Braverman alijiuzulu kutokana na ukiukaji wa data mara mbili.

Na yeye hakuenda kimya kimya, bali katika barua yake ya kujiuzulu, alisema alikuwa amefanya ukiukaji wa kiufundi kwa kutuma hati rasmi kutoka kwa barua pepe ya kibinafsi, na kwamba sasa anawajibika.

"Kujifanya kuwa hatujafanya makosa, kuendelea kana kwamba kila mtu haoni kuwa tumeyafanya, na kutumaini kwamba mambo yatakwenda sawa sio siasa kali," aliandika.

"Nimefanya makosa; nakubali kuwajibika; najiuzulu."

Ujumbe huo ulichukuliwa kama kumshambulia waziri mkuu mbele ya umma, ukimkosoa Truss na uongozi wake bila kumtaja jina.

Braverman pia aliibua wasiwasi mkubwa kuhusu dhamira ya serikali ya kuheshimu ahadi za ilani, kuhusu masuala kama vile uhamiaji.

**AFANANISHWA NA BOGA LETUSI**

Wakati mchambuzi wa masuala ya kisiasa alitania kwamba Truss alikuwa na takriban maisha sawa na Letusi, kwa maana ya muda wa kuhudumu, kulingana na gazeti la Uingereza la Daily Star.

Maelfu ya watu walitazama 'letusi', kando ya picha iliyowekwa kwenye fremu ya waziri mkuu.

Mboga iliponyauka taratibu mbele ya macho yao, ndivyo Truss naye alivyokuwa madarakani.

Na wakati Waziri Mkuu alipotangaza kujiuzulu, karibu watu 20,000 walianza kupongeza letusi kwa kuwa katika ubora wake kwa muda mrefu ikilinganishwa na muda ambao Truss amekuwa madarakani.

Giza lilipotanda jijini London, ilikadiriwa picha kubwa ya boga kwenye sehemu ya nje ya jengo la bunge la Westminster, kabla ya kutangazwa kwenye Twitter kwamba "letusi" imefika bungeni.

# Soko Mawasiliano linapogeuka janga

## • Wamachinga walikimbia, wengine walia ukata

**Na Sabato Kasika**

WAMACHINGA ni miongoni mwa wafanyabiashara muhimu katika usisimuaji wa uchumi wa nchi, na ndio maana serikali imekuwa ikiwaweka kipaumbele kwa kuwajengea maeneo mazuri ya kufanya shughuli zao.

Hatua ya kuwajengea masoko maalum inatokana na kuwapunguzia ugumu wa ufanyaji kazi zao kwa kutembea mitaani na barabarani kutafuta wateja, badala yake wanakaa katika eneo rasmi linalotambuliwa na serikali.

Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo za serikali, baadhi ya wafanyabiashara hao wamekuwa wakihamishwa na kisha kurudi katika mazingira waliyoondolewa wakitoa sababu mbalimbali za kufanya hivyo.

Soko la Mawasiliano lililopo Sinza Dar es Salaam, ambalo wafanyabiashara ndogondogo walilengwa, inaelezwa kukumbwa na mdororo baada ya sehemu kubwa ya wafanyabiashara kulikimbia.

Awali soko hilo lilojengwa kwa gharama kubwa, lilikuwa na wafanyabiashara 2,600, lakini kwa sababu mbalimbali wamebaki 964 kutokana na kundi kubwa kuondoka na kurudi kule walikoondolewa awali.

Makamu Mwenyekiti wa soko hilo, Mussa Mbwani, anataja sababu ya baadhi ya wamachinga kuondoka kuwa ni mtindo wa kufanya biashara kwa mazoea ambao unaweza kusababisha waendelea kuchuuza kwa kutembea.

"Kila mara katika masoko mbalimbali, wenzetu wamekuwa wakilalamika kwamba hayana miundombinu yote, na kwamba yamejengwa mbali ambako wateja hawawezi kufika, lakini hapa kuna kila kitu," anasema Mbwani.

Anasema soko hilo lina choo, maji na usafiri wa daladala kutoka maeneo mbalimbali ya jijini Dar es Salaam, na kwamba hakuna sababu ya mashiko ya kuwafanya wenzao waondoke, bali chanzo ni mazoea.

"Huko walikokwenda si salama, kwani wanapanga biashara zao kandokando ya barabara, lakini pia kila siku wanatozwa shilingi 1,000 wakiambiwa ni za ushuru, lakini zinaingia mifukoni mwa wajanja wachache," anasema.

Mbwana anafafanua kuwa ushuru wa kila siku unaochukuliwa na Manispaa ya Ubungo ni shilingi 500, na kwamba hao waliokimbia ni sawa na kuruka majivu na kukanyaga moto.

"Ninasema hayo kwa sababu maeneo yao yatachukuliwa na watu wengine, hivyo wakitimuliwa huko barabarani watakosa pa kwenda, hivyo watafakari na kisha wachukue hatua za kurudi sokoni," anasema.

**SOKO KUBORESHWA**

Wakati mwenyekiti huyo akisema hayo, tayari Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ameagiza Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kuboreshwa kwa soko hilo.

Maboresho hayo ni pamoja na kujenga vibanda kwa ajili ya wafanyabiashara kulingana na aina ya biashara ambazo wanafanya na pia vizimba viwe vya kuvutia wateja.

Mkuu huyo wa mkoa alitoa maagizo hayo hivi karibu, wakati wa ziara ya kusikiliza kero za wafanyabiashara katika soko hilo, huku akielekeza LATRA kuongeza ruti za daladala na TANESCO kushughulikia huduma ya umeme.

Wadau wengine waliopewa maelekezo na mkuu huyo wa mkoa ni DAWASA ambayo inatakiwa kufikisha huduma ya maji sokoni hapo na TARURA kuhakikisha inaboresha miundombinu ya soko.

Mfanyabiashara wa mboga katika soko hilo, Rahma Baraka, anaomba vibanda vya wamachinga waliohama kwenda kuchuuza barabarani, viondolewe kwa madai kwamba vinawaziba katika maeneo yao.

"Zamani wateja walikuwa wanakuja na magari yao hadi hapa katika mabanda ya Manispaa tunakofanyia biashara, lakini sasa yamezibwa na vibanda vya wauza mitumba ambap sasa hawapo, tunaomba viondolewe," anasema.

Rahma anafafanua kuwa zamani alikuwa anauza tenga la nyanya kwa siku mbili linaishia, na kwamba tangu wazibwe na vibanda hivyo, anaweza kukaa na tenga la nyanya kwa zaidi ya wiki moja.

"Kama hawaviondoi, basi vipangwe vizuri ili ziwepo barabara kwa ajili ya wateja wenye magari wapite na kutufikia huku ndani wanunue bidhaa, vinginevyo tutaendelea kuumia kwa kukosa wateja," anazidi kusema

**ZIWEPO BIDHAA ZA JUMLA**

Mfanyabiashara wa mahindi mabichi ya jumla, katika soko hilo, Ally Shaban anaomba wafanyabiashara wengine zaidi wa mazao ya jumla watumie soko hilo, kwa kuwa lina nafasi ya kutosha kutumiwa na magari ya mizigo.

"Yaani hapa kwa sasa mahindi mabichi ndio yanauzwa kwa bei ya jumla, tunaomba waje wafanyabiashara wa viazi vitamu, mviringo na mazao mengine ya jumla wahamie hapa," anasema Shaban.

Anasisitiza huduma zote za mazao ya jumla ikipatikana, soko hilo litachangamka na litapata wateja wengi wanaotaka bidhaa za jumla badala ya kwenda kwingine ikiwamo Mabibo na Tandale.

"Soko hili lipo eneo zuri, linafikika, ila shida moja tu ya kutokuwapo kwa bidhaa za jumla, hivyo niwaombe wafanyabiashara wenzangu wanaouza mazao kwa bei ya jumla wahamie hapa," anasema.



Baadhi ya meza za wafanyabiashara ziko wazi katika soko hilo. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**



Makamu Mwenyekiti wa soko la Mawasiliano, Mussa Mbwani

# Miaka 50 inayoibeba NBAA Afrika

## ▪Yawa muhimili kwa mataifa mbalimbali

Na Joseph Mwendapole

MWAKA huu Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), imetimiza miaka 50 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1972.

Bodi hiyo imefikisha umri huo ikiwa na mafanikio mengi yaliyoifanya kupata sifa lukuki kitaifa na kimataifa kutokana na umahiri wake kwenye fani hiyo.

Upekee huo ndio umewavutia mataifa mbalimbali kuja kujifunza na kutuma watumishi wake kuja kujifunza masuala ya uhasibu na ukaguzi hapa nchini.

Hatua ya Tanzania kupata sifa kimataifa kwenye fani ya uhasibu ni jambo la kupongezwa kwani mpaka kufikia hatua hiyo menejimenti ya NBAA bila shaka imefanya kazi kubwa.

Tanzania na Nigeria zimetajwa kuwa nchi pekee barani Afrika zinazotumia viwango vya kimataifa kwenye uhasibu na ukaguzi hali inayozifanya nchi hizo kuwa mfano kwa mataifa mbalimbali duniani.

Gazeti hili lilifanikiwa kuzungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, CPA Maneno Pius ambaye ameelezea mafanikio mengi tangu kuanzishwa kwa bodi hiyo na matarajio ya baadae.

Maadhimisho yameanza mwezi wa nane na yanatarajiwa kufikia kilele mwezi Novemba mwaka huu na wakati wa maadhimisho hayo kutakuwa na shughuli mbalimbali za kijamii.

"Katika mafanikio ya kimataifa sisi tumekuwa wanachama wa Shirikisho la Wahasibu Duniani (IFAC) na ni mwanachama mwanzilishi wa Shirikisho la Wahasibu Afrika (PAFA) na Tanzania ni moja ya nchi zinazoheshimika sana duniani kwenye masuala ya uhasibu na ukaguzi," anasema

" Afrika kuna nchi mbili tu, Tanzania na Nigeria zinazotumia viwango vya kimataifa vya uhasibu na ukizungumza chochote hata kwenye mkutano wa IFAC utaambiwa nenda Tanzania ukajifunze," anasema

Anasema, kutokana na umahiri huo Tanzania imeingia kwenye makubaliano ya miaka mitano na Serikali ya Msumbiji kwaajili ya kuwafundisha watumishi wake utawala bora katika usimamizi wa fedha.

Anasema wataalamu hao wamekuwa wakifundishwa hapa nchini na wakati mwingine wataalamu wa Tanzania wanalazimika kwenda nchini humo kwaajili ya kutoa mafunzo hayo.

"Tunawafundisha Msumbiji kwasababu wanataka kuwa kama sisi, Malawi, Zambia nao wamekuja wanataka tushirikiane kwenye eneo hili la uhasibu na ukaguzi ili waweze kuwa kama sisi," anasema Mkurugenzi huyo

Anaeleza katika shamrashamra hizo, NBAA imeandaa shindano la uandaaji wa hesabu bora kwa makampuni, taasisi na mashirika mbalimbali.




Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), CPA Pius A. Maneno akiwa kwenye picha ya Pamoja na wafanyakazi wenzake

Mkurugenzi huyo anasema wameandaa mashindano mbalimbali ambapo washindi watajizolea zawadi akitaja moja ya mashindano hayo kuwa ni kwa yule atakayeandaa hesabu bora.

Anasema makampuni, wizara idara za serikali halmashauri zinaalikwa kuleta hesabu zao zilizokaguliwa na zilizotayarishwa kuanzia mwezi wa nane hadi Novemba ambazo watazichambua na mshindi aliyetengeneza hesabu vizuri atapata zawadi.

Mkurugenzi huyo anaongeza kwamba kwenye tuzo hizo kutakuwa na mkutano mkuu wa wahasibu ambao hufanyika kila mwaka na watazungumzia masuala mbalimbali yanayohusu taaluma ya uhasibu.

"Tutajadili masuala mbalimbali yanayohusiana na maslahi ya umma na pia namna gani ya kuendeleza taaluma hii ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu na kwenye mkutano huo tutaangalia maadili ya taaluma yetu," anasema

Anasema katika miaka yake 50, NBAA imefanya mambo mengi makubwa ikiwamo kusajili wahasibu na wakaguzi na mpaka sasa waliofaulu mitihani ya bodi hiyo wanafikia 26,000 na kati ya hao, 12, 000 walifaulu katika ngazi ya CPA na 14,400 katika ngazi ya watunza vitabu vya hesabu.

"Pia tumesajili kampuni 450 za kutengeneza hesabu na ukaguzi haya ni maendeleo makubwa sana ndani ya miaka 50 ya NBAA, tumetunga viwango vya kutayarisha hesabu za fedha kwa sekta binafsi na kwa sekta ya umma" anasisitiza

Aidha, anafafanua kuwa wamefanikiwa kutengeneza kanuni za maadili ya wahasibu na wakaguzi na kuandaa semina na makongamano kila mwaka kitaifa na kimataifa.

Anasema, mwaka hivi karibuni NBAA ilifanikiwa kuandaa mikutano zaidi ya 17 kwa wanachama wake pamoja na mashirika ikiwamo Benki Kuu Tanzania (BoT), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Aidha, katika mafanikio hayo wamejenga kituo cha taaluma maeneo ya Bunju, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam (Accountancy Profession Center) (APC) na moja ya kumbi hizo inauwezo wa kuchukua hadi watu 1,000 na ndogondogo zinachukua watu 400 hadi 500.

Anafafanua kuwa wanachama wa bodi hiyo wamekuwa washauri wakuu wa wafanyabiashara na wenye makampuni kuhusu namna bora ya kutunza fedha katika makusanyo na matumizi ili waweze kulipa kodi wanazostahili.

"NBAA imeingia kwenye makubaliano ya kushirikiana kwenye kazi za kitaaluma na Nchi za Afrika Mashariki na Chama ha Wahasibu cha India wanachoshirikiana kwenye semina na makongamano mbalimbali ya kitaaluma," anazidi kusema mkurugenzi huyo..

Hata hivyo, Bodi hiyo imefanikiwa kushinda tuzo ya mwajiri bora mara mbili Mkoa wa Dar es Salaam hali ambayo inaonyesha ushirikiano mzuri baina ya menejimenti na watumishi wa ngazi mbalimbali za bodi.

Anataja mafanikio mengine kuwa ni serikali kusikiliza ushauri wao pale wanaposhauri sehemu za kupunguza kodi au kuongeza.

"Kwenye mafanikio changamoto hazikosekani ingawa sisi tunazichukua changamoto kama fursa na changamoto ni waajiri na kampuni kutozingatia viwango vya hesabu kama tunavyotaka sasa inatuletea kashfa," anasema

Anasema wamekuwa wakitoa adhabu kwa watu wanaoandaa hesabu zisizozingatia viwango na kuwapa mafunzo ya aina mbalimbali kwaajili ya kuwawezesha kuandaa hesabu zenye viwango.

"Kumekuwa na tatizo la baadhi ya wahasibu kutengeneza hesabu za aina tatu, moja yenye faida kubwa kwaajili ya kuombea mkopo benki, yenye faida ya kati kwa matumizi yao na yenye faida ndogo kwajili ya kupeleka TRA ili wakadiriwe kodi ndogo kitu ambacho siyo sahihi," anasema

"Watu wa aina hii tukiwabaini kama ni wanachama wetu tunawanyanga'nya vyeti kwasababu kama ilivyo kwenye vyuo cheti siyo mali yako ni mali ya seneti ukifanya makosa wanakunyang'anya nasisi hapa NBAA tunakunyang'anya kwasababu tunazingatia uadilifu," alisema

Aanasisitiza NBAA inajitahidi kuwapa wanachama wake kupata mafunzo yanayojitosheleza ili wafanye kazi vizuri kusaidia waajiri wao kuandaa hesabu nzuri zenye viwango.



TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Vituko, historia ya sanamu la 'Bismin'

## • Zamani kama hujaliona, hujafika Dar
## • Wengine waliiamkia, wakiogopa bunduki

**Na Adam Fungamwangwo**

MAKUTANO ya barabara ya Samora na Azikiwe, mitaa ya Posta kuna sanamu moja kubwa jeusi lililo juu kwa jukwaa au jiwe kubwa.

Sanamu inamuonyesha mtu mweusi akiwa amevaa shati na kaptula, ameshika bunduki.

Sanamu hiyo imeupa mgongo upande wa Magharibi na bunduki yake imeelekezwa upande wa Mashariki, baharini ambako inatoka kuelekea barabara ya Azikiwe, huku ya Samora ikiwa inapita ubavuni mwake. Eneo la mduara ambapo magari yanapita kushoto kila upande, katikati yake kuna bustani ndogo.

Kwa miaka ya hivi karibuni naona kama kizazi cha sasa hakifuatilii au kutaka kujua historia ya sanamu hilo, siyo kwa nini limewekwa pale tu, lakini lilivyokuwa likitetemesha watu wengi, hasa waliokuwa wanatoka mikoani.

Miaka ya 1990 kurudi nyuma, sanamu hilo lilikuwa maarufu zaidi Dar es Salaam kuliko kitu chochote kile.

Hadi leo inabaki kuwa ndiyo nembo ya Dar es Salaam. Ukiwa unaiongelea Dar hata kwenye televisheni bila kuonyesha sanamu hiyo inakuwa kama hujaiongelea vizuri.

Watu waliokuwa wanatoka mikoani na kufikia kwa ndugu zao moja ya sehemu ambazo walikuwa wanaomba wapelekwe ni kuiona sanamu hiyo ambayo ilijichukulia umaarufu mkubwa nchini.

Miaka hiyo sijui kwa nini walikuwa hawaiiti sanamu ya Bismin, ila ilijulikana kama 'picha ya Bismin.'

Kwa miaka hiyo hakuna mtu yoyote kutoka mikoani ambaye anaweza kuaminika kama amefika jijini Dar es Salaam kama hajaiona sanamu hiyo.

Anaporudi kijijini na kuulizwa inabidi awe na ushahidi wa kutosha kama kweli alikwenda Dar kwa kujibu maswali kadhaa ambayo wenzake watathibitisha kuwa kweli amefika.

Kufika Dar hasa kwa watu wa mikoani hakikuwa kitu cha mchezo mchezo hasa kutokana na miundombinu ya wakati huo. Dar ilionekana iko mbali mno, na pia ilionekana kama vile mtu anapokwambia anakwenda au anatoka Ulaya.

Moja ya vitu ambavyo wengi waliofika Dar ambavyo walikuwa wakiulizwa wanaporejea, na ndiyo wanavyotaka kupelekwa na kutembezwa na ndugu zao ni sanamu ya Bismin, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa ambao kwa sasa unaitwa Julius Nyarere, Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Kivukoni, Hospitali ya Muhimbili, na klabu za Simba na Yanga.

Kwa uchache ukipata hata nusu ya hivi nilivyovitaja, na ukawa na ushahidi hata kama siyo wa picha ila maneno tu, ukajibu maswali yao vizuri, basi wewe kijijini utatamba na watu watakuheshimu kuwa umefika Dar es Salaam.

Katika vitu vyote hivyo, ilikuwa rahisi sana kwa mgeni kumpeleka kwenye sanamu ya Bismin kwa sababu sehemu mabasi kutoka sehemu zote jijini yalikuwa yakishia Kariakoo au Posta.

Sasa vituko vinakuja pale vijana au watoto watukutu wanapowapeleka wenzao wanaotoka mikoani kwenye sanamu hilo wanavyowatisha.

Wanapofika pale wanawaambia waiamkie, la sivyo ile bunduki itafyatuliwa na kumuua. Hiyo ilisababisha wengi wakati huo waliorejea kijijini au waliobaki hapa hapa Dar, lakini waliotoka vijijini kuiamkia sanamu hiyo.

Ni moja ya sanamu iliyopata 'shikamoo' nyingi wakati huo. Waliaminishwa kama sanamu ile ina uhai, na yule ndiye mwenye mji wa Dar es Salaam, asipomwamkia atapigwa bunduki au kurudishwa kijijini au mkoa alikotoka.

Wengine walipigishwa magoti kabisa na kuambiwa amwambie 'mzee shikamoo' na wakafanya hivyo.



Sanamu ya askari mweusi kuwakilisha mwafrika aliyepigana vita kuu ya kwanza ya dunia lililopo maeneo ya Posta Dar es Salaam maarufu kama 'picha ya Bismin'.



Sanamu ya Gavana wa zamani wa Ujerumani nchini, Herman Von Wissman kabla ya kuwekwa la sasa.

Mbinu hiyo ilitumiwa na 'watoto wa mjini' kuwaingiza mjini waliotoka 'bushi' kwa sababu wengi wao inadaiwa walikuwa wakilizoea jiji wanajifanya wajuaji zaidi kuliko wenyeji.

Kwa hiyo huwa anakumbushwa kuwa asijifanye mjuaji sana au mjanja wakati wao ndiyo wamemuonyesha mji, kiasi kwamba walimpeleka hadi kwenye 'picha ya Bismin' na kuiamkia. Hiyo humfanya mjuaji anywee na kuwa baridi kama maji ya mtungini. Kwa nini sanamu ile imewekwa pale? Na ni nini? Na kwa nini ikawa ndiyo nembo ya Dar es Salaam?

Historia yake inaanza mwaka 1889, kabla na baada ya Vita Kuu ya kwanza ya Dunia.

Kwa ufupi sanamu ya mwanzo kukaa pale ni sanamu ya Herman Von Wissman, Gavana wa Kijerumani ambaye anakumbukwa kwa kutekeleza utekaji na mauaji ya Abushir Ibn Salim Al Harthi, mtawala na sultani wa Pangani Tanga.

Baada ya kumteka na kumyonga Abushir, Von Wissman alirejea Ujerumani na kisha baadaye kuteuliwa kuwa Gavana wa Nchi zilizokuwa chini ya Ujerumani za Afrika Mashariki.

Alifanya utafiti wa kutafuta ni wapi kitovu cha mji wa Dar es Salaam, yaani katikati ya Dar es Salaam au Mzizima wakati huo tena kwa vipimo, ndipo alipogundua sehemu ile ndiyo katikati ya Dar wakati ule. Hii ina maana bado sehemu kubwa ya Dar ya sasa ilikuwa pori, nafikiri mwisho upande wa Magharibi ilikuwa ni Manzese, na Mashariki na kuvuka Kigamboni halafu kuna Kariakoo, Ilala, Magomeni, na Msasani.

Wissman alisimamisha sanamu yake mwaka 1909, nadhani ndiyo maana wengi wakawa wanaifahamu kwa jina la 'picha ya Bismin' hasa Waswahili wakati huo, wakishindwa kutamka Wissman.

Baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia iliyopiganwa kuanzia mwaka 1914 hadi 1918, Waingereza walishinda na kuchukuwa koloni la Tanganyika, ndipo mwaka 1916 sanamu la Bwana Von Wissman liliondolewa na likawekwa Sanamu la sura ya askari mweusi Mwafrika katika sare ya kijeshi ya King's African Rifles wakati wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia (1914-1918) akishika bunduki yenye kisu cha kando na kutazama upande wa bahari mwaka 1927 Hii ilikuwa ni kama ishara ya kuthamini Waingereza kutambua mchango wa Askari Waafrika waliopigana kwenye Vita hivyo. Sanamu imedumu hadi leo hapo panapoitwa Askari Monument Garden, Posta Dar es Salam.

**Tuma meseji 0716 350534**

## Wagombea uwaziri mkuu Uingereza kuanza kampeni

**LONDON, Uingereza**

WAGOMBEA wanaowania uwaziri mkuu wa Uingereza kufuatia hatua ya Liz Truss kujiuzulu juzi, wanatarajiwa kuanzisha kampeni za kutafuta uungwaji mkono mwishoni mwa wiki.

Hata hivyo, vyama vya upinzani nchini humo vimetaka uchaguzi mkuu uitishwe, raia wamchague Waziri Mkuu mpya na kumaliza miezi kadhaa ya mvutano wa kisiasa nchini humo.

Miongoni mwa wanaopigiwa upatu kuwania wadhifa huo ni waziri mkuu wa zamani ambaye pia aliondolewa madarakani Boris Johnson na Rishi Sunak aliyeshindwa na Truss katika kinyang'anyiro kilichopita.

Wachambuzi wa siasa nchini humo walisema, chama cha Conservative kinapaswa kumpata kiongozi atakayekiunganisha chama badala ya kukigawa zaidi.

Truss alijiuzulu baada ya kukaa madarakani kwa siku 45 kufuatia mpango wake wa kiuchumi kusababisha mtikisiko katika masoko ya fedha

**DW**

## UN kupiga kura kuinusuru Haiti

**NEWYORK, Marekani**

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa linapanga kupiga kura kuhusu azimio ambalo litataka machafuko ya Haiti na visa vingine vya uhalifu nchini humo kukomeshwa.

Azimio hilo pia linalenga kumwekea vikwazo Jimmy Barbecue Cherizer, kiongozi wa magenge ambaye anaungwa mkono.

Marekani na Mexico ambazo ziliandaa azimio hilo, zilichelewesha upigaji kura tangu Jumatano ili ziweze kulipitia tena kwa lengo la kutafuta uungwaji mkono wa wanachama wote 15 wa baraza hilo.

Azimio hilo limemtaja Jimmy Barbecue Cherizer ambaye genge lake limezuia kituo kikubwa cha mafuta hivyo kusababisha uhaba mkubwa wa bidhaa hiyo.

Ikiwa azimio hilo litapitishwa basi Cherizer ambaye ni ofisa wa zamani wa polisi na anayeongoza muungano wa magenge ujulikanao kama familia ya G9, atawekewa vikwazo kadhaa vya usafiri, vya silaha na mali yake kukamatwa.

Haiti inaandamwa na misukosuko ya kisiasa tangu kuuawa kwa Rais Jovenel Moise mwaka uliopita.

**DW**

# Hofu yatanda tishio kulipuliwa bwawa Kherson

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, ameishutumu Russia kwa kujiandaa kulipua bwawa katika kiwanda cha kuzalisha umeme wa maji kusini mwa nchi hiyo hatua itakayosababisha maafa.

Katika hotuba yake ya usiku kiongozi huyo, alisema bwawa la Kakhovka kwenye mto Dnieper lilikuwa limechimbwa na vikosi vya Russia, kulingana na habari za Ukraine.

Bwawa hilo liko chini ya uvamizi wa Russia, lakini vikosi vya Ukraine vinalikaribia.

Russia tayari imeishutumu Ukraine kwa kurusha makombora kwenye bwawa la Kakhovka.

Bwawa hilo pia huipatia Russia mojawapo ya njia chache zilizosalia kuvuka mto Dnieper katika eneo linalokaliwa la Kherson.

Mamlaka zilizowekwa na Russia huko Kherson zimekataa madai ya Ukraine ya njama ya kuharibu muundo huo.

Walilaumu vikosi vya Ukraine kwa shambulio kwenye kivuko kingine muhimu, Daraja la Antonivskiy.

Watu wanne waliuawa, akiwemo mkuu wa kituo cha televisheni, maofisa hao walisema.

Russia ilianza kuwahamisha wakala wake huko Kherson wiki hii lakini pia ilisema raia 50 hadi 60,000 wataondoka pia, hatua hiyo ilishutumiwa kuwa kama kufukuzwa kwa lazima na mamlaka ya Ukraine.

Kamanda mpya wa jeshi la Russia nchini Ukraine, Jenerali Sergei Surovikin, alidai kwamba vikosi vya Ukraine vinaweza kuwa vinapanga njia zilizopigwa marufuku za vita katika mji wa Kherson na bwawa la kuzalisha umeme na aliongeza kwamba inahalalisha uhamishaji wa raia.

Ukraine yaomba msaada Israel

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Dmytro Kuleba alifanya mazungumzo kwa njia ya simu na waziri mkuu wa Israel Yair Lapid, akiomba nchi hiyo kusaidia mifumo na teknolojia za ulinzi wa anga.

"Nilimweleza kuhusu mateso yasiyoelezeka, kupoteza maisha na uharibifu unaosababishwa na makombora ya Russia na ndege zisizo na rubani zilizotengenezwa Iran. Tulijadili kwa kina ombi letu kutupa mifumo na teknolojia kwa ajili ya ulinzi wa anga na makombora," alisema waziri huyo kupitia Twitter.

Licha ya kulaani uvamizi wa Russia, Israeli inakataa kuipatia Ukraine silaha, ikielezea katika kudumisha ushirikiano na Russia juu ya masuala yanayohusiana na vita vya Syria na kwa maslahi ya ustawi wa Wayahudi wanaoishi nchini humo.

Usaidizi wa Israel kwa Ukraine ni mdogo katika utoaji wa misaada ya kibinadamu. Hivi karibuni, serikali ya Israel imejitolea kusaidia katika kuendeleza mfumo wa onyo wa mashambulizi ya anga kwa raia.

Ikizungumzia mazungumzo hayo, huduma ya vyombo vya habari ya Lapid ilisema kwamba kiongozi huyo kwa mara nyingine alionyesha kuunga mkono Ukraine, na pia alizungumzia wasiwasi kuhusu uhusiano wa kijeshi kati ya Russia na Iran.

Wanajeshi wa Russia wametumia makumi ya ndege zisizo na rubani za Kamikaze kwenye miundombinu muhimu ya Ukraine. Serikali ya nchi hiyo inadai kwamba Russia inatumia ndege zisizo na rubani za Shahed-136 zilizotengenezwa na Iran.

Iran inakanusha kupelekwa kwa ndege hizo nchini Russia. Ikulu ya Kremlin pia ilisema wanajeshi wa Russia hawatumii ndege zisizo na rubani za Iran nchini Ukraine.

Marekani ilizitaja kauli za Tehran kuwa ni za uongo.

***BBC***



Moto unaoambatana na moshi ukionekana juu ya barabara baada ya waandamanaji kuweka kizuizi kwa kuchoma matairi wakati wa maandamano nchini Chadi. **PICHA: AFP**

# Chad vurugu inazidi kusambaa

**N'Djamena, Chad**

KUMEKUWA na lawama za kimataifa kuhusu ghasia za hivi karibuni za nchini Chad, ambapo waandamanaji 50 waliuawa na wengine 300 kujeruhiwa katika maandamano ya kuunga mkono demokrasia.

Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya na Marekani zimetoa wito kwa pande zote kujitenga, lakini wanachama wa upinzani wameapa kuendelea kuandamana.

Katika hali isiyo ya kawaida, ubalozi wa Marekani nchini Chad sio tu ulitoa taarifa ya kulaani ghasia za Alhamisi, lakini pia ulichapisha picha kwenye mitandao yake ya kijamii, ikimuonyesha balozi huyo akiwa amepiga magoti karibu na nguo zilizokuwa na damu mitaani.

Haya yalijiri baada ya watu waliokuwa wamevalia kama raia kuondoa vizuizi na kuua watu wanne nje ya geti la ubalozi huo.

Haijabainika kwa nini ubalozi wa Marekani ulilengwa.

Amri ya kutotoka nje imetolewa katika mji mkuu Ndjamena na miji mingine mitatu ambako maandamano yalifanyika. Wanachama wa upinzani walisema maandamano yataendelea hadi matakwa yao yatakapotekelezwa.

***BBC***

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa ipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kuwanyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-2

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Enock, mwenzio jana nilikamatwa nikapelekwa kwenye nyumba ya Usonzo."

"Unasemaje Mary?" Enock alishtuka.

"Nimekuja kuchukuliwa kwa nguvu hapa nikapelekwa kwa tajiri."

"Kwa nini?"

"Mhh, kwani hujui kuwa ananitaka?"

"Kwani si anajua kuwa una mchumba?"

"We lile baba si unalijua? Linatumia utajiri wake kurubuni na kutisha wasichana."

"Sasa ikawaje?"

"Wee mimi tena, nimempa makavu huko huko, ooh mimi nakupenda nataka nikuoe, nikamwambia. wee nini? Sitaki nakwambia." Wakati akiongea hivyo Enock akaangua kicheko, halafu akamkatisha.

"Usinidanganye Mary, wewe yule Usonzo umemjibu maneno hayo akuache kweli na ukatili wote ule?"

"Unafikiri aliniacha? Kwanza ile nafika tu, akanishika nywele zangu hizi rasta akanivuta na kuanza kuniambia maneno hayo, eti we mtoto kwa nini kila siku nakwambia nakupenda, lakini wewe huonyeshi ushirikiano. Si unajua kila akiniambia nakataa, sasa naona amekasirika na anatumia nguvu. Sikuogopa wala nini, nikamwambia sikutaki, akanisukuma, nikaanguka chini puu, sikuinuka hadi akawaambia wanirudishe. Unajua aliona aibu nimemkataa mbele ya wasaidizi wake na mimi nilifanya makusudi."

"We Mary wewe, unajua unajiweka kwenye hatari, yule si mtu mzuri, ni mtesaji na muuaji."

"Sasa kwa sababu hiyo nimkubali? Nimuogope kwa sababu ana pesa na anaua watu?"

"Hapana, sijasema umkubali, ila umjibu tu kwa ustaarabu na upole, unajua matajiri huwa hawapendi kuona kama wanadharauliwa, tena na watu kama sisi."

"Ni kweli lakini mimi nitamheshimu kama atakuwa na adabu, lakini akiendelea na tabia hii mimi nitamwambia tu, simuogopi na wala siogopi kufa."

************************************

Mosha alikosa raha. Pamoja na kwamba kwenye mpango wake huo wa kuchukua ardhi ya wanakijiji alijipatia pesa nyingi kwa kukusanya mazao na kwenda kuyauza Dar es Salaam, akiwachia visenti tu wananchi, lakini kitendo cha kumkosa Mary kwake ilikuwa ni muhali.

Alipokutana na Mwenyekiti wa Kijiji mzee Chale alilalamika kuhusu jambo hilo.

"Kiongozi hapa tupo kwenye kusaka pesa bwana, wanakijiji tumeshawaweka sawa, tumewatapeli ardhi wamelalamika lakini kwa sasa wamezoea, leo tena unataka kufanye magumashi ili umpate huyo binti kusema kweli hii siyo sahihi. Kwa sababu itaibua upya hisia za wanakijiji. Hili lenyewe hapa wamenyamaza tu kwa sababu tuna sungusungu wa kuwatisha na wakati mwingine kuua kama ikilazimika, kwa hilo mimi hapana. Wewe ni tajiri mwenye pesa, fanya ushawishi wako ili binti akukubali, lakini siyo kulazimisha, kumteka au kufanya kitu chochote kibaya, hapana," mzee Chale alimpasha Usonzo. Akabaki mdogo kama pilitoni.


"Kwanza yule ana mchumba wake."

"He, kumbe ana mchumba?"

"Ulikuwa hujui?"

"Humu humu kijijini?"

"Ndiyo, anaitwa Enock, huyo ndiye mchumba wake. Kijiji kizima kinajua, sasa eti wewe unanze tena kumfuatafuata mchumba wa watu haiwezekani na mimi hapo sitokuwa pamoja na wewe. Mimi nipo pamoja nawe kwenye huu mradi wetu wa kupiga pesa, lakini siyo kwa hilo, sikuungi mkono."




> **"Mimi kama kiongozi wenu na mwekezaji tutajitahidi kurekebisha hali hiyo, kwa hiyo msiwe na wasiwasi wananchi." Mzee Chale aliwapoza.**

Wiki moja baadaye ulifanyika mkutano mkubwa wa kijiji na viongozi wake, ambapo wanakijiji waliomba kuongezwa pesa za mazao kwa sababu wanashindwa kujikimu kimaisha ikikumbukwa kuwa robo tatu ya ardhi yote imechukuliwa na mwekezaji.

"Mimi kama kiongozi wenu na mwekezaji tutajitahidi kurekebisha hali hiyo, kwa hiyo msiwe na wasiwasi wananchi." Mzee Chale aliwapoza.

Wakati mkutano unamalizika, Usonzo na mwenyekiti mzee Chale waligundua kuna kitu ambacho si cha kawaida.

Ni kwamba wanawafahamu wanakijiji wote na idadi yao, lakini ni kama waliona kuna sura ya mtu mpya kwenye mkutano ule. Wakaanza kujiuliza ni nani? Pamoja kwamba alionekana ni wa kawaida tu asiye na makeke na alikuwa anapiga makofi kuwaunga mkono muda wote, lakini walitaka tu kujua ni nani.

Kwa kawaida mtu yoyote ambaye ana madhambi, huwa makini sana ili asijulikane, au kuamini sana watu ili kuficha mambo yake.

Wakampa kazi mmoja wao ili kufanya uchunguzi wa mgeni yule ni nani na amekuja kwenye kijiji kile kufanya nini.

Baada ya siku mbili taarifa ilipelekwa kwa mwenyekiti mzee Chale na mwekezaji Usonzo kuwa mgeni yule anaitwa Adel Adam, mwenye miaka 30 hivi. Jamaa huyo ametoka Dar es Salaam akitumwa na wazazi wake kumchukua bibi yake mzaa mama bibi Anna Msafiri ambaye ni mgonjwa ili akapate matibabu bora jijini.

Kwa sababu yote wanamfahamu bibi Anna na jinsi ambavyo kwa sasa ni mgonjwa, presha ikawashuka kuwa hakuwa mtu ambaye anaweza kutibua mipango yao kama walivyodhani.

***********************************

Awali hakutaka kabisa kuifanya kazi ile. Lakini yeye ndiye alikuwa mkubwa, ndugu zake aliofuatana nao kuzaliwa walikuwa ni wanawake, hivyo mama yake alimwambia kama asipokwenda basi hakukuwa tena na mtu wa kwenda kumchukua bibi yake ambaye ni mgonjwa.

"Bibi yako ni mgonjwa sana, kwa hiyo mimi na baba yako tumekuchagua wewe uende nyumbani. Uende kijijini Maweni ukamchukue bibi yako. Tunaona kama kule inawezekana matibabu ni ya shida kuliko huku. Hapa anaweza kupata matibabu ya uhakika na kwa uwezo wa Mungu atapona," akamkumbuka mama yake jinsi alivyomuagiza.

Akamuonya pia kutojiingiza kwenye migogoro isiyomhusu.

"Kule ni kwetu sisi, mimi na baba yako tumetoka kule, lakini wewe na ndugu zako mmezaliwa Dar, kule hamjulikani sana, tangu mko wadogo mlikuwa mnakwenda wakati wa likizo tu, kwa hiyo ukifika huko ujiepushe sana na mambo yasiyokuhusu."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# WASHINDI BETIKA MTOKO WATUA KUSHUHUDIA DABI

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuonyesha mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga ni mchezo mkubwa nchini, mashabiki wa timu hizo kutoka nje ya Dar es Salaam walioibuka vinara wa promosheni ya Mtoko wa Kibingwa wamewasili jijini ili kushuhudia dabi hiyo kwa gharama za Betika.

Mashabiki 48, nusu wakiwa ni kutoka nje ya Dar es Salaam wataishuhudia dabi hiyo, ukiachana na ule utani wa jadi, lakini kila mmoja atakuwa na mtu wake wa karibu aliyemchagua kushuhudia mchezo huo wakigharamiwa na kampuni hiyo ya michezo ya kubashiri.

Mashabiki hao waliwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jana tayari kuangalia dabi hiyo itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Hawa ni wale ambao waliibuka washindi, waliweka beti kuanzia mechi saba na kuendelea wakaingia kwenye droo ya wiki ili kushinda promosheni ya Mtoko wa Kibingwa," alisema Nelson Mwanuzi, ambaye ni Ofisa Makoso wa Betika.

Mwanuzi alisema promosheni hiyo tayari imepata washindi 24 wakitokea Dar es Salaam na idadi kama hiyo wakitoka mikoa tofauti hapa nchini.

"Washindi kutoka nje ya Dar es Salaam wamewasili leo 'jana' kwa ndege na kesho 'leo' kutakuwa na bata la msimu, ambayo ni pati kubwa ya kuwakaribisha Dar es Salaam washindi hao," Mwanuzi alisema.

Aliongeza pati hiyo itakuwa na watu maarufu nchini, wachambuzi na wasanii, ambayo lengo lake ni kuwapa mabingwa hao burudani ya msimu mpya wa dabi, kabla ya kuishuhudia uwanjani.

Akizungumzia dabi hiyo, Nelson alisema kabla ya mechi kesho, leo, washindi hao hawataboreka, wakati wakiisubiri dabi hiyo, watapata kitu kingine cha tofauti cha bata la msimu, wakiwasikiliza wachambuzi mbalimbali laivu wanavyoichambua mechi na nafasi ya timu zao kupata ushindi.

Aliongeza katika bata hilo, mashabiki wa Simba watakuwa na vaibu lao vivyo hivyo kwa wale wa Yanga, lengo likiwa ni kuinogesha zaidi wakati wakisubiri dakika 90 za kibabe Jumapili, Betika ikigharamia.

Alisema kuhusu Mtoko wa Kibingwa, Nelson amesema hii ni mara ya nne ambapo mara ya kwanza ilikuwa Juni, 2021 kwa washindi saba na baadaye Novemba mwaka huo walileta mashabiki 15.

"Tofauti na misimu mingine, safari hii vionjo vimeongezeka kwa shabiki kumchagua mtu wake wa karibu wa kuambatana naye katika mechi hii, ambaye atagharamiwa pia na Betika.

Baadhi ya washindi hao walisema hiyo ni mara yao ya kwanza kufika Dar es Salaam.

"Sikuwahi kuwaza kuishuhudia dabi hii laivu, Betika imenifanyia jambo kubwa," alisema, Julius Kiria kutoka Ruvuma.

Aliwataja baadhi ya washindi kutoka nje ya Dar es Salaam na watu wao wa karibu kwenye mabano kuwa ni Moses Andrea (Simon Mwanfeya), Abraham Mandala (Jimmy Joseph), Erick Mongi (Anzuruni), Erasto Margwe (Meckson Martin), Frank Haule (Lueiegad Njovu), Dennis Changanyikeni (Abdul Said), Ally Salum (Jacquiline Mkandala), Felix Charles (Frank Bushaijabwe) na Jevon Mhaluka (Adam Khalfani).



Ofisa Habari wa Kampuni ya Betika, Juvenalius Rugambwa (watatu kulia), akiwa na mashabiki wa Simba na Yanga kutoka mikoa mbalimbali ambao wametua jijini, Dar es Salaam kwa ajili ya kushuhudia mechi ya watani wa jadi itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba Queens vs Yanga Princess leo

**Na Saada Akida**

WAKATI macho na masikio ya wapenzi wa soka hapa nchini yakisubiri kuona na kusikia mchezo wa watani wa jadi kati ya Yanga na Simba unaotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, dada zao, Simba Queens na Yanga Princess zitakutana leo katika mechi maalum ya Tamasha la Tanzanite itakayochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru.

Mechi hiyo ni sehemu ya Kongomano la Michezo la Wanawake lililoandaliwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwa kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa lengo la kuongeza hamasa kwa wanawake nchini kujitokeza kwa wingi kushiriki michezo.

Pia kutakuwa na mechi ya utangulizi kati ya Fountain Gate Princess dhidi ya Baobab Queens zote kutoka jijini, Dodoma. Mara ya mwisho timu hizo kukutana ilikuwa Aprili 24, mwaka huu ambapo Yanga Princess iliibuka na ushindi wa bao 1-0 mchezo wa marudiano wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu uliopita.

Simba Queens wanaikabili Yanga wakiwa na kocha mpya raia wa Uganda, Charles Lukula, ambaye atatumia mchezo huo kama maandalizi ya mwisho kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayoanza rasmi Oktoba 30, mwaka huu nchini Morocco.

# Matumaini Simba Queens Afrika

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba kupitia mlezi wa Simba Queens, Fatema Dewji, ameipongeza timu hiyo na kuwataka kwenda kupambana katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ya wanawake itakayofanyika kuanzia Oktoba 30 hadi Novemba 13, mwaka huu nchini Morocco.

Katika hatua nyingine viongozi wa Simba wametoa zawadi kwa baadhi ya wachezaji waliofanya vizuri katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa CECAFA ambapo, Vivian Corozene aliyekabidhiwa pikipiki aliibuka Mchezaji Bora.

Kipa bora katika mashindano hayo alikuwa ni, Gelwa Yona ambaye alipewa televisheni huku beki bora, Esther Mayala na Kiungo Bora, Joelle Bukuru pia walipata zawadi.

Akizungumza katika halfa fupi iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, Fatema alisema anawapongeza wachezaji kwa mafanikio waliyopata na anaamini wakakwenda Morocco kupeperusha vyema bendera ya klabu.

Fatema alisema wachezaji walifanya kazi kubwa sana katika michuano ya CECAFA na anaamini pia watafanya vizuri katika michuano iliyopo mbele yao.

"Ninaimani kubwa ya kufanya vizuri kwa sababu ya ubora wao licha ya ugumu wa michuano hiyo, kwa kufanya kile ambacho walikifanya katika michuano ya CECAFA na kuhamisha nguvu zaidi ya mashindano ya Afrika," alisema Fatema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah (Try Again) alisema anaimani ya timu hiyo inakwenda kufanya vizuri kama ilivyo kwa kaka zao.

"Leo hatutakuwa na maneno mengi kikubwa siku ya leo kuwapongeza, ninaimani kubwa na wachezaji kile mlichokifanya katika CECAFA, mtaenda kushindana katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Try Again.

Simba Queens itafungua michuano hiyo kwa kucheza dhidi ya wenyeji ASFAR FC mchezo utakaopigwa Oktoba 30, mwaka huu halafu itakutana na Determines Girls ya Libya hapo Novemba 2 na Novemba 5, mwaka huu itamaliza mechi za hatua ya makundi kwa kuikabili Green Buffaloes kutoka Zambia.

## ZISIKUPITE

### RONALDO KULIPA FAINI
MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo anakabiliwa na faini ya pauni milioni moja na klabu hiyo baada ya kuondoka mapema uwanjani katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Tottenham Hotspur. ***(Star)***

### LUKAKU KUBAKIA INTER
KLABU ya Chelsea ipo tayari kumruhusu mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, kusalia kwa mkopo Inter Milan msimu ujao kabla ya kufutilia mbali mamilioni ya pauni kwa kumuuza. ***(Gazzetta dello Sport, via Mirror)***

### PALACE KUMUUZA DIAZ
KLABU ya Crystal Palace inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Blackburn na Timu ya Taifa ya Chile, Ben Brereton Diaz mwenye umri wa miaka 23. ***(Sun)***

### NDICKA ANUKIA ARSENAL
KLABU ya Arsenal inaweza kujaribu kumsajili beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Evan Ndicka mwenye umri wa miaka 23, kutoka Eintracht Frankfurt Januari. ***(Standard)***

### MILAN YAMTAKA BROJA
KLABU ya AC Milan inavutiwa na mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 21. ***(Calciomercato)***

### VATA AGOMBEWA ULAYA
ARSENAL, Manchester City, Juventus, Roma na AC Milan wanavutiwa na kiungo wa kati wa Celtic na nyota wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland mwenye umri wa miaka 17, Rocco Vata. ***(Tuttomercatoweb)***

### UNITED KUMWACHIA RONALDO
KLABU ya Manchester United inaweza kumwachia mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 kuondoka bure ifikapo Januari. ***(inews)***

### DIAZ AKARIBIA SEVILLA
KLABU ya Sevilla inaongoza kwenye mbio za kumwania, Brereton Diaz katika dirisha dogo la Januari ***(Football Insider)***

### MADRID, PSG, CITY VITANI
REAL Madrid, Paris St-Germain na Manchester City zimetuma maskauti kumtazama winga wa Napoli na Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 21. ***(90min)***

### LOBOTKA ANUKIA EPL
KIUNGO wa Slovakia, Stanislav Lobotka mwenye umri wa miaka 27 anatazamiwa kusaini mkataba mpya na Napoli, licha ya kunyatiwa na Arsenal, Liverpool na Tottenham. ***(90min)***

### BASSEY ALITAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal ilikuwa na nia ya kumsajili beki wa Nigeria, Calvin Bassey mwenye umri wa miaka 22, kutoka Rangers msimu wa joto - kabla ya kuhamia Ajax. ***(Own Goal Nigeria).***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI AFUNGUKA BAADA YA USHINDI

**Asema matokeo mazuri aliyopata juzi ni majibu kwa wakosoaji ambao…**

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi anaamini timu yake iliwajibu wadau wanaoikosoa kwa kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Villarreal kwenye mechi ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, iliyochezwa juzi akisema "ilibidi nichukue hatua".

Blaugrana hao walipata ushindi huo kwa mabao mawili ya Robert Lewandowski na Ansu Fati akafunga la tatu pale kwenye dimba la Camp Nou.

Ushindi huo unamaanisha Barca wamepitwa pointi tatu na vinara wa ligi hiyo, Real Madrid baada ya kufungwa kwenye El Clasico mwishoni mwa wiki.

Wakiwa na ushindi mmoja pekee katika mechi nne zilizopita kabla ya ushindi wa Alhamisi, Xavi alikiri timu yake ilihitaji kujibu wakosoaji wao, na alifurahi walifanya hivyo kwa mtindo wa kuvutia.

"Tulicheza mchezo mzuri," alisema. "Ilikuwa zamu yetu (ya kushinda), tulipaswa kufikia. Haikuwa rahisi, kwa sababu mengi yalitarajiwa kutoka kwetu baada ya matokeo mabaya.

"Kuna matarajio mengi yaliyowekwa juu yetu msimu huu. Lakini tulionyesha sura yetu halisi, tulionyesha tabia. Ni hisia nzuri kwa ujumla."

"Tuna uchovu miongoni mwa wachezaji wetu. Tunahitaji nguvu na tunahitaji ubora wetu. Wachezaji lazima waunganishwe, kwa dakika wanazocheza."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,042,0
MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 2.09
X | 3.37
2 | 3.27
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GERRARD ATIMULIWA ASTON VILLA



**LONDON, England**

ASTON Villa imethibitisha, Steven Gerrard ameachana na klabu hiyo mara moja baada ya kufungwa na Fulham.

Kipigo cha Craven Cottage kilikuwa cha hivi punde zaidi katika safu ya matokeo duni kwa Gerrard, ambaye amesimamia ushindi mmoja wa Ligi Kuu England katika mechi nane.

Villa sasa wako katika nafasi ya 17 katika msimamo wa Ligi Kuu England, juu ya eneo la kushushwa daraja kwa mabao ya kufunga.

Awali Gerrard alikuwa kocha wa Rangers, ambapo alishinda taji la Ligi Kuu Scotland kabla ya kumrithi Dean Smith kama kocha wa Aston Villa Novemba, mwaka jana.

Taarifa ilisema: "Tunapenda kumshukuru Steven kwa bidii na kujitolea kwake na tunamtakia heri kwa siku zijazo."

Msaidizi wa Gerrard, Michael Beale, aliondoka Villa Park majira ya joto na kuwa Kocha wa Queens Park Rangers.

# Lukaku hataki kurudi Chelsea

**MILAN, Italia**

GAZETI la Gazzetta Dello Sport limeripoti mshambuliaji wa Inter Milan, Romelu Lukaku hataki kurejea Chelsea, hivyo wako tayari kuongeza mkopo wake hadi mwaka 2024 na kisha kufanya uhamisho wake kuwa wa kudumu.

Mshambuliaji huyo wa Ubelgiji alirejea Inter msimu uliopita wa joto baada ya kipindi cha kutatanisha cha mwaka mmoja huko Stamford Bridge ambapo aliwasili msimu wa joto wa 2021 kama usajili ghali zaidi katika historia ya klabu.

Hata hivyo, alishindwa kuhalalisha bei yake ya euro milioni 115 akifunga mabao nane pekee katika mechi 26 za Ligi Kuu England akiwa chini ya Thomas Tuchel.

Lukaku alirejea Inter kwa mkataba wa mkopo msimu uliopita, ikimaanisha kuwa Inter hawana chaguo au wajibu wa kununua.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Gazzetta, wababe hao wa Serie A na Chelsea wana makubaliano ya kiungwana ya kuongeza muda wa kukaa kwa Lukaku hapo hadi 2024.

Inter italipa euro milioni 10 kwa mkopo mwingine wa msimu mmoja, ikijumuisha mshahara wa mshambuliaji na kujaribu kujumuisha chaguo la kununua katika mpango huo.



## HABARI MICHEZO

026,796/-

# MUUZA MBAO ASHINDA BONUS YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA ya mbao, anayetokea Mufindi wilaya ya Mafinga, Iringa, Maliki Mshuza, ameshinda Sh. milioni 15.6 katika Jackpot Bonus ya Sportpesa iliyochezwa katikati ya wiki iliyoisha, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya mechi 13.

Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za Sportpesa jijini Dar es Salaam, Maliki alisema alianza kucheza na Sportpesa katikati ya mwaka 2021, akiwa hakumbuki mwezi kamili.

"Nilianza kucheza na Sportpesa mwaka mmoja uliopita. Unajua pale ninapoishi kuna watu wengi wanacheza michezo ya kubashiri, hivyo walinishawishi lakini nilichukua muda kidogo kukubaliana nao kama na mimi nianze kubashiri kama wao.

Kwa mujibu wa maelezo yake, Maliki anasema kila jioni mara nyingi alikuwa anawaona vijana wenzie mmoja mmoja ama kwa vikundi wakikaa pamoja wanaonyeshana simu na mara nyingine wanafurahi pamoja au wanasononeka kwa pamoja.

Lakini mara nyingi alikuwa akiwaona wakifurahia hivyo na yeye kwa sababu alikuwa karibu yao wakawa wanamshawishi kwa nini na yeye asiweke bashiri zake kama wao.

"Mimi sichezi Multibet au single bet. Mimi nacheza hizi Jackpot tu. Mazoea yangu kila mkeka ukitoka mara nyingi huwa najipa siku tatu nachambua timu taratibu usiku kabla ya kulala nikiwa nimetulia".

Maliki anasema akishaweka mkeka huwa hafuatilii mikeka yake kuitazama kwenye TV au kwa kutumia app za matokeo kwa sababu hataki presha. "Mimi nikishaweka mkeka huwa nauacha mpaka mechi ziishe ndipo nakuja kuangalia matokeo.

Naye Meneja Uhusiano na Mawsailiano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Maliki kwa ushindi na kumtaka aendelee kupambania ndoto zake za kuibuka na Jackpot za SportPesa bila kuchoka. Hivi sasa Jackpot kubwa ya SportPesa imefikia Sh. bilioni 1.04.

"Kipekee nikupongeze kwa uamuzi wako wa kucheza Jackpot. Kama ambavyo leo umetoa ushuhuda umeanza kucheza rasmi mwaka jana na sasa umevuna matunda kwenye Jackpot bonus, basi nikutakie kila la kheri kwenye ndoto zako," aliongeza Sabrina.




Mshindi wa Jackpot bonus, Maliki Mshuza kutoka Mafinga, Iringa akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 15.6 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. Jackpot kubwa wiki hii ni Sh. bilioni 1.04. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/10/22 | 17:00 | Everton vs Crystal Palace | 2.46 | 3.19 | 2.89 |
| 02. 22/10/22 | 17:00 | Sunderland vs Burnley | 2.88 | 3.23 | 2.45 |
| 03. 22/10/22 | 17:00 | Sheffield Utd vs Norwich City | 2.55 | 3.25 | 2.75 |
| 04. 22/10/22 | 17:00 | Millwall vs West Bromwich | 2.78 | 3.23 | 2.53 |
| 05. 22/10/22 | 17:00 | Reading vs Bristol City | 2.40 | 3.24 | 2.94 |
| 06. 22/10/22 | 20:00 | Niort vs Dijon | 2.73 | 3.18 | 2.68 |
| 07. 22/10/22 | 21:30 | Arminia Bielefeld vs St. Pauli | 2.89 | 3.44 | 2.33 |
| 08. 23/10/22 | 14:30 | Karlsruher SC vs Fortuna Dusseldorf | 2.34 | 3.43 | 2.89 |
| 09. 23/10/22 | 16:00 | Wolverhampton vs Leicester | 2.25 | 3.38 | 3.08 |
| 10. 23/10/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Brest | 2.41 | 3.27 | 2.87 |
| 11. 23/10/22 | 16:00 | Troyes vs Lorient | 2.42 | 3.37 | 2.78 |
| 12. 23/10/22 | 17:15 | Betis vs Atletico Madrid | 3.08 | 3.23 | 2.32 |
| 13. 23/10/22 | 17:30 | CS Maritimo vs FC Arouca | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 14. 23/10/22 | 19:30 | Girona vs Osasuna | 2.58 | 3.08 | 2.83 |
| 15. 23/10/22 | 20:00 | GD Chaves vs Gil Vicente | 2.45 | 3.34 | 2.79 |
| 16. 23/10/22 | 21:45 | Lille vs Monaco | 2.46 | 3.52 | 2.63 |
| 17. 23/10/22 | 21:45 | Roma vs Napoli | 2.83 | 3.47 | 2.36 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 22/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2846 | Nizhny Novgorod vs FC Krasnodar | 2.98 | 3.42 | 2.21 |
| 14:00 | 3930 | M. Nam Dinh vs CLB BD Thanh Hoa | 2.96 | 3.54 | 2.09 |
| 14:00 | 4592 | BFC Daugavpils vs Spartaks Jurmala | 2.21 | 3.50 | 2.77 |
| 14:15 | 3884 | Pusamania Borneo vs PSS Sleman | 1.67 | 3.44 | 4.75 |
| 14:30 | 1340 | Hearts vs Celtic | 7.61 | 5.20 | 1.33 |
| 14:30 | 1371 | Tallinna Kalev vs Tallinna JK Legion | 1.92 | 4.10 | 2.98 |
| 14:30 | 2771 | Nottingham vs Liverpool | 9.94 | 5.96 | 1.23 |
| 14:30 | 3123 | Khon Kaen United FC vs Buriram Utd | 7.99 | 5.07 | 1.29 |
| 15:00 | 3183 | Rayo Vallecano vs Cadiz CF | 1.73 | 3.49 | 4.89 |
| 16:00 | 2964 | Geita Gold FC vs Namungo | 2.05 | 2.87 | 3.80 |
| 16:00 | 5266 | Salernitana vs Spezia | 1.98 | 3.36 | 3.61 |
| 16:30 | 1935 | Bayer Leverkusen vs VfL Wolfsburg | 1.66 | 4.05 | 4.34 |
| 16:30 | 3845 | Borussia Dortmund vs Stuttgart | 1.48 | 4.47 | 5.56 |
| 16:30 | 4190 | SC Freiburg vs Werder Bremen | 1.88 | 3.72 | 3.57 |
| 16:30 | 4226 | Hoffenheim vs Bayern Munchen | 5.16 | 4.86 | 1.47 |
| 16:30 | 5375 | Augsburg vs RB Leipzig | 5.13 | 4.24 | 1.54 |
| 17:00 | 1752 | Everton vs Crystal Palace | 2.48 | 3.08 | 2.83 |
| 17:00 | 3305 | Trabzonspor vs Sivasspor | 1.61 | 3.99 | 4.88 |
| 17:00 | 3838 | Manchester City vs Brighton | 1.23 | 5.84 | 10.62 |
| 17:00 | 4975 | Dila Gori vs Dinamo Tbilisi | 4.18 | 3.25 | 1.81 |
| 17:15 | 2553 | Valladolid vs Real Sociedad | 3.46 | 3.31 | 2.09 |
| 17:30 | 2708 | Feyenoord vs Fortuna Sittard | 1.19 | 6.75 | 10.91 |
| 18:00 | 1069 | Montpellier vs Lyon | 3.83 | 3.83 | 1.81 |
| 18:00 | 4568 | Pafos FC vs Omonia Nicosia | 2.04 | 3.30 | 3.60 |
| 18:30 | 5242 | Legia Warszawa vs Pogon Szczecin | 2.10 | 3.26 | 3.16 |
| 19:00 | 1119 | Atromitos vs Volos | 2.21 | 3.29 | 3.14 |
| 19:00 | 1723 | Denizlispor vs Altinordu | 2.30 | 3.16 | 2.87 |
| 19:00 | 1920 | AC Milan vs Monza | 1.37 | 4.86 | 6.95 |
| 19:00 | 2599 | Odd Ballklubb vs Valerenga | 2.93 | 3.57 | 2.20 |
| 19:00 | 4723 | Lokomotiv Moscow vs Dinamo Moscow | 2.57 | 3.41 | 2.52 |
| 19:00 | 5520 | Ham-Kam vs Stromsgodset | 2.03 | 3.43 | 3.43 |
| 19:15 | 4652 | Flint Town United vs Airbus UK Broughton | 1.70 | 4.00 | 4.30 |
| 19:30 | 1580 | Valencia vs Mallorca | 1.74 | 3.45 | 4.89 |
| 19:30 | 3360 | Tammeka Tartu vs Parnu JK Vaprus | 1.50 | 4.28 | 5.05 |
| 19:30 | 4059 | Panetolikos vs Olympiakos | 5.58 | 4.09 | 1.54 |
| 19:30 | 4573 | Chelsea vs Manchester Utd | 2.09 | 3.37 | 3.27 |
| 19:30 | 5144 | Puskas Akademia vs Ferencvaros TC | 3.41 | 3.31 | 1.98 |
| 19:30 | 5444 | Monchengladbach vs Eintracht Frankfurt | 2.21 | 3.66 | 2.82 |
| 19:45 | 3608 | Waalwick vs Ajax | 8.90 | 6.33 | 1.24 |
| 20:00 | 1249 | Apoel Nicosia vs AEK Larnaca | 2.10 | 3.30 | 3.45 |
| 20:00 | 2500 | Fenerbahce vs Basaksehir | 1.91 | 3.58 | 3.68 |
| 20:00 | 3825 | GD Estoril vs Sporting Braga | 4.39 | 3.79 | 1.71 |
| 20:30 | 2933 | Backa Topola vs Cukaricki St | 1.77 | 3.40 | 4.17 |
| 21:00 | 2082 | Maastricht vs Den Bosch | 2.36 | 3.59 | 2.61 |
| 21:00 | 3758 | Rakow Czestochowa vs Korona Kielce | 1.16 | 6.21 | 13.59 |
| 21:00 | 4090 | Dordrecht vs NAC Breda | 2.80 | 3.49 | 2.26 |
| 21:45 | 5459 | Fiorentina vs Inter | 3.48 | 3.38 | 2.02 |
| 22:00 | 2090 | Real Madrid vs Sevilla FC | 1.37 | 4.91 | 7.22 |
| 22:00 | 3149 | Marseille vs Lens | 2.01 | 3.39 | 3.54 |
| 22:30 | 4753 | Belenenses vs Benfica Lisbon B | 2.71 | 3.36 | 2.39 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Serengeti Girls kazi moja India

INATOKA UK. 32

Katika hatua nyingine, Ngorongoro Heroes itaingia kambini leo kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kushiriki mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON U-20)zitakazofanyika mwakani nchini Misri.

Tanzania imepangwa Kundi B ikiwa na Uganda na Ethiopia huku Kundi A likiwa na Sudan, Sudan Kusini, Djibouti na Burundi, ili kupata timu mbili zitakazoiwakilisha CECAFA kwenye fainali hizo.

# Simba yabadili gia

INATOKA UK. 32

jificha baada ya kuona wanashindwa kupata matokeo, wanasema hawajiandai sana. Ukweli wanajiandaa kweli kweli na mechi dhidi yetu," alisema Kamwe.

Aliongeza mbinu ya kuwafanya wabweteke waione ni mechi ya kawaida kama wanavyotaka kuwaaminisha mashabiki wao ili wawashtukize wameibaini.

Hivi karibuni, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alikaririwa akisema jinsi watani zao wa jadi wanavyojiandaa na mechi hiyo kama wanacheza fainali za Kombe la Dunia au hawatocheza tena mechi yoyote ya mpira wa miguu.

"Wenzetu hii ndiyo mechi yao kubwa kwenye maisha yao ya mpira, hili ndiyo Kombe la Dunia kwao, mechi hii ndiyo mashabiki, viongozi, wachezaji na wanachama wanaitolea macho na wanakamia kama hawachezi tena katika maisha yao," alisema Ahmed.

Katika hatua nyingine, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limemtangaza mwamuzi wa kimataifa, Ramadhani Kayoko kwa kushirikisha na Mohammed Mkono, Janeth Balama na Elly Sassii ndio watasimamia mechi hiyo.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 22, 2022

Nipashe



UKURASA 30

## Gerrard atimuliwa Aston Villa



Manahodha wa Simba Queens, Fatuma Issa (kulia) na Oppah Clement (kushoto) wakimkabidhi Kombe la ubingwa wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Mlezi wa timu hiyo, Fatema Dewji (katikati), katika sherehe maalumu iliyofanyika jijini, Dar es Salaam jana. Wengine katika picha ni viongozi wa Klabu ya Simba. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba yabadili gia, Yanga yawashtukia

### ●●●Vigogo hao waendeleza tambo kuelekea dabi ya kesho, Kayoko...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikisema imejipanga kuhakikisha inalipa kisasi kwa kuwafunga watani zao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho, Yanga imeweka wazi wameshtukia propaganda inayoenezwa na Mnyama haufikirii mchezo huo kwa sababu wao ni 'next level'.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah (Try Again), alisema timu yake imejipanga kuonyesha kwa vitendo usemi wa "Mkapa hatoki mtu" watakapokutana na Yanga hapo kesho.

Try Again alisema wanajivunia ubora wa kikosi walichonacho huku akiongeza wamejipanga vizuri kuonyesha ukubwa wa Simba na kauli mbiu hiyo sasa imehamia kwenye michezo dhidi ya timu za hapa nyumbani.

Alisema, licha ya kupoteza mechi iliyopita, haina maana wao ni dhaifu sana mbele ya Yanga na kesho wataonyesha kile wanachokifanya katika michezo ya kimataifa dhidi ya timu kubwa.

"Simba sio 'underdog' mbele ya Yanga, mara nyingi mechi za dabi zinakuwa na mambo mengi, tumejipanga vizuri na Jumapili tunaenda kuendeleza usemi wetu kwa Mkapa hatoki mtu katika mechi hiyo kwa mara ya kwanza.

Msimu uliopita tulifungwa mara tatu, hiyo haimaanishi Simba ni mateja mbele ya Yanga, katika mchezo wa dabi kunakuwa na mambo mengi na tunapofanya makosa wenzetu wanayatumia kutuhukumu," alisema Try Again.

Aliongeza wamejiandaa vizuri na Wanasimba waendelee kuonyesha mshikamano na kusapoti timu yao ili kuhakikisha wanaendelea kukusanya pointi muhimu katika mchezo huo.

"Tutafanya vizuri, wala hatupati tabu katika ligi licha ya kupoteza taji msimu uliopita, tunaenda kupata matokeo mazuri katika mchezo huo, Simba ni mafahari, presha hatuna na tumechukua tahadhari zote za mchezo wetu wa Jumapili," alisema mwenyekiti huyo wa bodi ya Wekundu wa Msimbazi.

Aliongeza kuwa viongozi wa klabu hiyo wanatarajia kukutana na wachezaji wao kwa ajili ya kuwajenga kisaikolojia pamoja na kuwapa hamasa kuelekea mchezo huo ambao wanaimani kubwa wachezaji na benchi la ufundi litawapa furaha mashabiki wa klabu hiyo.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema hawawezi kubweteka kufuatia kauli zinazotolewa na wapinzani wao kuwa 'hawaitolei macho' mechi hiyo si za kweli na wanafanya hivyo ili kuwapumbaza.

Kamwe alisema Yanga inajiandaa kikamilifu kuwakabili Simba kama ambavyo hujiandaa kucheza 'dabi' nyingine zilizopita.

"Kwenye ligi zote duniani kuwa 'dabi' na hata kama timu moja ni dhaifu na nyingine ina uwezo mkubwa kama Liverpool na Everton, lakini timu zote huwa zinajiandaa kikamilifu, ila mwisho wa siku ubora ndiyo unaamua.

Yanga tunajua mchezo huu ni mkubwa sio Tanzania, bali Afrika na wenzetu hawajiandai au walikuwa hawajiandai huko nyuma, hii ni propaganda ambayo wameileta, wametafuta kichaka cha ku-

INAENDELEA UK. 31

## Serengeti Girls kazi moja India

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA itaandikwa leo saa 8:00 mchana kwa saa za Tanzania wakati Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls) itakapovaana na Colombia katika mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia, ikisaka rekodi nyingine ya kutinga hatua ya nusu fainali.

Mechi hiyo itacheza kwenye Uwanja wa Pandit Jawaharlal Nehru, Goa, nchini India inapofanyika michuano hiyo.

Tanzania ambayo ilishika nafasi ya pili kwenye Kundi D, inacheza dhidi ya Colombia ambao walikuwa vinara katika Kundi C kwa kujinyakulia pointi sita.

Kocha wa Serengeti Girls, Bakari Shime, alisema maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika, huku akisema wachezaji wake wamekuwa wakipanda viwango katika kila mechi waliyocheza na anaamini utakuwa mchezo mzuri na wenye ushindani.

"Hali ya hewa ya huku haina tofauti na ya nyumbani kwa wakati huu, pia wachezaji wangu kila mechi viwango vinazidi kuongezeka, kwa hiyo naamini mechi itakuwa ngumu, lakini tunaweza kufanya vizuri, tunaomba tu Watanzania wazidi tukuombea ili tuendelee kuweka historia," alisema Shime.

Aliongeza mechi zote katika michuano hiyo ni ngumu kwa sababu kila upande ulifanya maandalizi mazuri kabla ya kufika India.

"Tunawaheshimu na tutacheza kwa tahadhari zaidi, tumedhamiria kuendelea kuipa heshima nchi yetu, ninaamini wachezaji wangu watacheza kwa bidii, watajituma na hawatakubali kupoteza kirahisi," Shime alisema.

Iwapo Tanzania itashinda leo itaendelea kuishangaza dunia, bali itaweka rekodi ambayo haijawahi kupatikana katika historia ya soka nchini.

Wakati huo huo, kikosi cha Tanzania cha umri chini ya miaka 23, kitashuka dimbani kuwakaribisha wenzao kutoka Nigeria katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Afrika (AFCON U-17).

Tanzania ilisonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuiondoa Sudan Kusini kwenye hatua ya awali.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >